SPORTPESA APP
CHEZA, USHINDE. MALIPO FASTA






**MUUGUZI** hospitali ya wilaya jela miaka 3 kwa kumwomba mgonjwa rushwa 200,000/-

UK.7




UKURASA 11


# Nipashe

Jumatatu Agosti 23, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580681

www.ippmedia.com

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710


## YALIYOMO


UKURASA WA 2

**WAHAMIAJI HARAMU WANASWA KWENYE GARI LILILOBEBA KABICHI**

WAHAMIAJI haramu 38 raia wa Ethiopia wamekamatwa na Idara ya Uhamiaji wilayani Handeni mkoani Tanga, wakiwa wamejificha ndani ya gari lililobeba kabichi wakielekea Afrika Kusini ...

UKURASA WA 3

**UAMUZI MDOGO LEO KESI YA KINA SABAYA**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, leo inatarajia kutoa uamuzi mdogo wa kukubali au kukataa maelezo yanayodaiwa kuandikwa kituo cha polisi na shahidi wa pili wa utetezi Silvester Nyegu (26), kutumiwa na Wakili wa Serikali kumhoji shahidi huyo...

UKURASA WA 7

**EWURA KUPUNGUZA MASHARTI UANZISHAJI VITUO VYA MAFUTA**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (EWURA), inatarajia kuanzisha mpango maalum wa kupunguza masharti ya kuanzisha vituo vya mafuta katika maeneo ya vijijini ili kupunguza tatizo ...


# Gwajima: Nitasema ukweli

*Endelea Uk. 2*



## Zitto asema hatokubali uteuzi serikalini

UKURASA 3



Askofu Dk. Edward Mwaikali

# Waumini wamshusha Askofu KKKT madhabauni

UK. 2


**MICHEZO** WATATU KUTUWAKILISHA OLIMPIKI AIBU - SAMIA UK.23

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Gwajima: Nitasema ukweli

**Na Elizabeth Zaya**

MBUNGE wa Kawe (CCM), Askofu Josephat Gwajima, amesema leo atafika katika Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuitikia wito wa Ofisi ya Bunge uliomtaka kufika mbele ya kamati hiyo.

Amesema ataitikia wito huo na kwamba atakwenda kueleza kila kitu kwa kusimamia ukweli kama imani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) inavyoeleza kwamba 'nitasema ukweli daima fitina kwangu mwiko'.

Askofu Gwajima aliyasema hayo jana Dar es Salaam wakati akiendesha ibada katika kanisa lake la Ufufuo na Uzima lililoko Ubungo.

Kwenye ibada hiyo, Askofu Gwajima alisema amejiandaa kusema ukweli mtupu mbele ya kamati hiyo na kwamba atakwenda kueleza mbele ya kamati hiyo, masuala mengineyo ambayo hajayasema sehemu yoyote.

"Kama mlivyoona kwenye mitandao, nilipata barua kutoka ofisi ya Spika kwamba Jumatatu ya kesho (leo), ninaitwa kwenye Kamati ya Maadili na Uongozi wa Bunge. Kwa hiyo kesho (leo) nitakwenda, wategemee kusikia ukweli. Mojawapo ya imani ya CCM inasema 'nitasema kweli daima, fitina kwangu ni mwiko," alisema Askofu Gwajima.


Aliongeza: "Na nitaongezea na mengine ambayo sijayasema, nitayasema yale ambayo mmeyasikia ni kweli, na kuna mambo mengine ambayo hamjayasikia, nayo nitawajazia kwa sababu ndiyo mtu wa Mungu anatakiwa kuwa hivyo na ndiyo maisha yanatakiwa kuwa hivyo, lazima tusimamie nchi na watoto wetu."

Kadhalika, Askofu Gwajima alisema hapingani na Rais Samia Suluhu Hassan kama watu wanavyojaribu kutengeneza na kupindisha na kwamba ukweli wake (yeye) anamkubali, anamheshimu, anampenda na ni kiongozi mzuri.

"Nimekuwa nikirudia maneno haya mara nyingi kwa sababu kuna baadhi ya watu wanapindisha maneno kwamba Askofu Gwajima anampinga Rais aaa...wapi, ukweli ni kwamba namkubali Rais Samia, ni kiongozi mzuri, ana upendo sana na ana huruma, " alisema Askofu Gwajima.

Agosti 21, mwaka huu Ofisi ya Bunge kupitia Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa ya ofisi hiyo, ilitoa taarifa ya wito kwa wabunge wawili wa CCM, Askofu Gwajima pamoja na Mbunge wa Ukonga, Jerry Silaa, kufika mbele ya kamati hiyo kujibu tuhuma mbalimbali zinazowakabili.

Miongoni mwa tuhuma zinazowakabili wabunge hao wa CCM zilizoelezwa na ofisi hiyo ya Bunge ni pamoja na kudaiwa kusema uongo na kushusha hadhi na heshima ya Bunge.



Baadhi ya wanafunzi wa Shule ya Sekondari Mugango, wilayani Musoma, mkoani Mara, wakijifunza somo la Kemia kwa vitendo katika maabara ya shule hiyo, mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wanaodaiwa kuwa wahamiaji haramu wanaswa kwenye gari lililobeba kabichi

**Na Hamida Kamchalla,** HANDENI

WAHAMIAJI haramu 38 raia wa Ethiopia wamekamatwa na Idara ya Uhamiaji wilayani Handeni mkoani Tanga, wakiwa wamejificha ndani ya gari lililobeba kabichi wakielekea Afrika Kusini.

Ofisa Uhamiaji wilayani Handeni, Joan Ndumbati, amethibitisha kutokea kwa tukio hilo na kusema kuwa, lilitokea Agosti 19, mwaka huu.

Ndumbati alisema awali walipata taarifa kutoka kwa wananchi kuhusiana na kuwapo gari la mizigo pembeni ya barabara ya shule, kuna watu wanashuka na hawaelewi wanatokea wapi na lengo lao ni nini.

Alisema askari wa uhamiaji kwa kushirikiana na viongozi wa kijiji na Kata ya Komkonga walifika eneo la tukio na kubaini uwapo wa raia hao wa Ethiopia, ambao idadi yao ilikuwa ni 50, lakini waliokamatwa ni 38 huku wengine 12 wakikimbilia katika shamba la katani lililokuwapo kwenye eneo hilo.

"Katika mahojiano na raia hao mmoja anaweza kuongea Kiswahili na kueleza kuwa wapo 50 wanatoka Ethiopia na kuelekea Afrika Kusini, ila tumebaini 12 wametoroka na kuingia kwenye shamba la katani la eneo hilo na juhudi za kuwatafuta na kuwakamata ili kufikishwa kwenye vyombo vingine vya kisheria zinaendelea," alisema Ndumbati.

Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Siriel Mchembe, alisema kwa mwaka mmoja sasa raia wa kigeni 110 wamekamatwa kwenye vizuizi mbalimbali vya barabarani wilayani humo, awali walikamatwa 72 na leo 38 huku wengine 12 wakiendelea kutafutwa baada ya kutoroka.

Mchembe aliongeza kuwa haipendezi viongozi kukosa taarifa muhimu kama hizo, hata kama ni raia wametoa taarifa ila ilipaswa ngazi husika kwenye vizuizi ndiyo wakamate watu hao, siyo mpaka gari liharibike au kuisha mafuta.

# Waumini KKKT wamshusha Askofu madhabauni

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MGOGORO unaofukuta ndani ya Kanisa La Kiinjili la Kilutheli Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Konde, umechukua sura mpya, baada ya waumini wa Kanisa hilo Ushirika wa Tukuyu Mjini kumkataa Askofu wa Dayosisi hiyo, Dk. Edward Mwaikali.

Mgogoro huo unatokana na Askofu Mwaikali pamoja na baadhi ya viongozi wa kanisa hilo kuhamisha Makao Makuu ya Dayosisi kutoka Tukuyu Mjini kwenda Mbeya Mjini jambo amblo baadhi ya waumini hawataki.

Kutokana na mgogoro huo, hivi karibuni Askofu Mwaikali pamoja na viongozi wengine wanaounga mkono kuhamishwa kwa makao makuu hayo, walianza kuwafukuza kazi wachungaji wanaopinga kuhamishwa kwa Dayosisi na kuwahamisha hamisha baadhi yao.

Taarifa zinadai kuwa zaidi ya wachungaji 20 wameshafukuzwa tangu mgogoro huo ulipoanza huku wengine kadhaa wakihamishwa kwenda katika maeneo tofauti tofauti.

Jana asubuhi, Askofu Mwaikali alifika katika Kanisa Kuu la Tukuyu wilayani Rungwe kwa lengo la kuendesha ibada na ndipo waumini wa kanisa hili wakakataa na kuanza kumzomea akiwa madhabauni, huku baadhi wakitoka nje ya kanisa.

Kutokana na hali hiyo, Askofu huyo anadaiwa kupiga simu polisi ndipo baadhi ya maofisa wa Jeshi la Polisi walipofika kanisani hapo na kuamua kumwondoa askofu huyo kanisani kwa ajili ya kurejesha hali ya usalama.

Baada ya askofu huo kuondolewa waumini hao walirejea kanisani na kuendelea na ibada huku wakiazimia kutomtambua Askofu Mwaikali kama kiongozi wao na kutopeleka sadaka jimboni pamoja na kuwarejesha kazini wachungaji wote waliofukuzwa.

Mmoja wa waumini wa kanisa hilo, Wasto Ngala, alisema wauminu kwa umoja wao walikataa Askofu Mwaikali kuendesha ibada kwa sababu hawamtambui kama kiongozi wao.

Alisema baada ya askofu huyo kuondoka wamekubaliana mambo manne, likiwamo la kutomtambua Askofu Mwaikali kama kiongozi wao na kutopeleka sadaka kwenye jimbo na dayosisi inayoshirikiana na Askofu Mwaikali.

Pia alisema walikubaliana kuwarejesha wachungaji wote zaidi ya 20 ambao waliandikiwa barua za kufukuzwa kazi na Askofu Mwaikali na washirika wake pamoja na kutompeleka mchungaji yeyote anayehamishiwa kwenye makanisa yao au kuruhusu mchungaji yeyote kuhamishwa.

**KAULI YA POLISI**

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya Kamishna Msaidizi wa Polisi, Ulrich Matei, alisema kilichotokea sio vurugu bali ilikuwa ni kutoelewana kati ya waumini wa kanisa hilo na askofu.

Alisema Askofu wa Kanisa hilo Dayosisi ya Konde pamoja na baadhi ya viongozi wanataka kuhamisha Makao Makuu ya Dayosisi kutoka Tukuyu kwenda Mbeya Mjini, jambo ambalo baadhi ya waumini hawakubali na kwamba ndicho chanzo cha kutoelewana.

Alisema katika eneo la kanisa hilo maofisa wa Jeshi la Polisi walikuwa wanafanya doria za kawaida kama ilivyo kwenye maeneo mengine, lakini hawakwenda kwa ajili ya kutuliza fujo kama ilivyoripotiwa na baadhi ya watu.

"Pale kanisani hakuna vurugu zilizotokea isipokuwa ni kutoelewana kati ya askofu na waumini ambao hawataki kuhamisha Makao Makuu ya Dayosisi ya Konde kuyapeleka Mbeya Mjini," alisema Kamanda Matei.

Alisema Jeshi la Polisi linaendelea kufuatilia mgogoro uliopo ndani ya kanisa hilo ili kuhakikisha havitokei vitendo vya uvunjifu wa amani ndani ya mkoa huo.

HABARI KITAIFA

# Zitto asema hatokubali uteuzi serikalini

**Na Gwamaka Alipipi**

KIONGOZI Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, ameweka wazi kuwa ikitokea akapata uteuzi wa wadhifa wowote serikalini, hataukubali, kwani kwa sasa ameweka nguvu na maono yake kwenye kujenga chama.

Alitoa kauli hiyo juzi kwenye mahojiano na kituo kimoja cha luninga baada ya kuulizwa kama ataafiki uteuzi wowote kama ilivyokuwa kwa aliyekuwa mshauri wa chama hicho, Prof. Kitila Mkumbo.

Akifafanua hoja hiyo, Zitto alisema: "Hapana nataka nijenge chama, huwezi kujenga taifa ukiwa na vyama goigoi, lazima uimarishe vyama vya siasa ili uwe na vyama madhubuti, vizae serikali madhubuti, kwa sasa hivi naona utume wangu siyo kuwa serikalini."

Aliongeza: "Utume wangu ni kuijenga ACT-Wazalendo kiweze kuwa chama imara, ambacho kinaweza kudhibiti mapigo ya aina yoyote na kinachoweza kuzalisha serikali itayoweza kuhudumia Watanzania vizuri.

Nitamshukuru Rais kwa imani yake kwangu, ila nitamwomba atafute mtu mwingine atakayeweza kuifanya kazi ambayo mimi ningeweza kuifanya, ili mimi nipate nafasi ya kujenga Chama cha ACT-Wazalendo."

Akizungumzia Uchaguzi Mkuu wa 2020, ambao ripoti yake ilikabidhiwa juzi kwa Rais Samia Suluhu Hassan kutoka Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Zitto alidai katika hali halisi hapakuwa na uchaguzi, bali operesheni ya kuturudisha kwenye mfumo wa chama kimoja.

"Binafsi sikushindwa uchaguzi wowote, nimefanya kazi kubwa sana Kigoma kipindi chote nilichokuwa kwenye siasa na nimependisha hadhi ya Mkoa wa Kigoma, Siyo kwamba wanaKigoma walinikataa. Ninaamini wapo wanaCCM wenye uwezo mkubwa ambao wangeshinda kihalali vilevile kama uchaguzi usingevurugwa," alisema Zitto.

Akijibu swali kuhusu tofauti ya utawala wa Rais Samia Suluhu Hassan na utawala uliopita, Zitto alisema kuna baadhi ya mambo Rais a Samia mebadilisha, alitolea mfano uhuru wa vyombo vya habari. Zitto aliongeza kuwa kuna baadhi ya mambo ambayo taifa lilitegemea yabadilike ila bado yako vilevile.

Aliongeza kuwa kuna umuhimu wa vyama vya siasa kukutana na Rais Samia kujadili namna ya kufanya siasa za hoja ili kuwe na mwelekeo mzuri.

## Uamuzi mdogo leo kesi ya kina Sabaya

**Na Allan Isack**, ARUSHA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, leo inatarajia kutoa uamuzi mdogo wa kukubali au kukataa maelezo yanayodaiwa kuandikwa kituo cha polisi na shahidi wa pili wa utetezi Silvester Nyegu (26), kutumiwa na Wakili wa Serikali kumhoji shahidi huyo.

Silvester Nyegu (26), Daniel Mbura na aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, wanakabiliwa na kesi ya jinai namba 105 yenye mashtaka matatu ya unyang'anyi wa kutumia silaha.

Agosti 20, mwaka huu hakimu mwandamizi wa mahakama hiyo, Odira aliahirisha kusikiliza kesi hiyo baada ya mawakili wa utetezi kupinga uhalali wa wakili wa Jamhuri kumhoji shahidi huyo kupitia maelezo yanayodaiwa aliandika kituo cha polisi.

Awali kabla ya kuahirishwa kwa shauri hilo, kulitokea mvutano wa kisheria kwa mawakili wa pande zote mbili hali iliyomlazimu hakimu kuahirisha kesi kwa dakika 15 kwenda kupitia hoja za mawakili hao.

Hakimu mwandamizi wa mahakama hiyo, alidai mahakamani kwamba baada ya kupitia hoja hizo, na kufanya uchunguzi wake hakufikia mwisho kwa kuwa jambo hilo halikuwa dogo kama mawakili hao walivyodhani.

"Katika kupekuwa na kupitia hoja zenu nimeona kuna maswali mengi yamejitokeza, hivyo tunaahirisha kusikiliza shauri hili hadi Agosti 23, mwaka huu nitatoa uamuzi mdogo kwa kuwa pande zote zipo kwa ajili ya kutafuta haki," alisema Hakimu Odira.

Akihojiwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Tumaini Kweka, shahidi huyo wa utetezi alidai mahakamani huko, kwamba hakuwahi kuandika maelezo yoyote kituo cha polisi wala kuhojiwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupata na Rushwa (TAKUKURU).

Katika hatua nyingine Wakili Kweka, aliiomba mahakama hiyo, kutumia kifungu namba 154 cha sheria ya ushahidi kutumia maelekezo ya shahidi aliyoandika kituo cha polisi kumhoji.




Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Omari Kumbilamoto (kulia), akikabidhi zawadi kwa mmoja wa wanawake nane kati ya 400, waliibuka washindi katika msimu wa pili wa kampeni ya mamalishe ya kuwaongezea thamani inayoendeshwa na kipindi cha MamaMia kupitia East Africa Radio na EATV, mkoani Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Meya Dar awafunda mamalishe washindi wa kampeni ya EATV

**Na Romana Mallya**

MEYA wa Jiji la Dar es Salaam, Omary Kumbilamoto, amewataka mamalishe walioibuka washindi katika msimu wa pili wa kampeni ya mamalishe ya kuwaongezea thamani inayoendeshwa na kipindi cha MamaMia kupitia East Africa Radio na EATV kuhakikisha vifaa walivyokabidhiwa vinakwenda kubadilisha maisha yao na ya wengine.

Meya Kumbilamoto aliyasema hayo juzi jioni wakati wa hafla ya kuwakabidhi wanawake nane kati ya 400 waliopendekezwa na wananchi katika maeneo yao kuwania katika msimu wa pili wa kampeni hiyo.

Kipindi hicho kinaendeshwa na watangazaji watatu ambao ni Maryam Kitosi ambaye ndiye kinara na msemaji wa masuala ya wanawake East Africa Radio na EATV, Ritha Chuwalo na Yusta Msowoya.

Katika msimu huu, mshindi ni Magreth Swai maarufu mama Neema anayefanya shughuli zake za mama lishe eneo la Tegeta ambaye amekabidhiwa pikipiki, jiko la gesi, unga, sukari, mchele, mafuta ya kupikia, kizimia moto pamoja na fedha Sh. 50,000.

Akizungumza katika hafla hiyo meya ambaye naye alitoa Sh. 200,000 kama zawadi kwa wanawake hao nane aliwataka washindi hao wakabadilishe maisha yao.

"Nilipata bahati ya kukutana na Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk. Reginald Mengi, wakati wa hafla ya kupokea ndege, akaniambia 'Mstahiki Meya, ukatae umaskini siyo vazi zuri la kulivaa, unaweza ukapambana na kutoka katika maisha' maana yake ni nini? Ukiangalia hizi bidhaa peke yake ukizitumia vizuri maana yake mmerahisishiwa maisha yenu," aliweleza.

Aliwatolea mfano wa kikundi cha wanawake watano ambao walifika ofisi kwake wakiomba kusaidiwa na walipewa fedha za mkopo ambazo baada ya mwaka walirudi lakini kila mmoja akiwa na kisingizio chake na hakuna aliyeweza kurejesha.

Alisema mnufaika wa kwanza wa mkopo alimpa mwenza wake fedha akamtolee mahari, mwingine akalipa madeni na wa tatu alikwenda kujenga chumba kimoja kwa sababu alikuwa anaishi nyumba ya kupanga.

Alisema mnufaika wa nne alikwenda kununua simu janja ya macho matatu na wa mwisho walikwenda kufanya dogori ikiwa ni agizo la baba yao aliyelitoa kabla hajafariki. Aliwaambia wanawake hao kuwa katika halmashauri mbalimbali zipo fursa za mikopo iliyotolewa na serikali kwa wanawake hivyo waangalie namna ya kuichangamkia ili kuzikuza biashara zao zaidi lakini kwa kuepuka kuwa kama hao wanawake watano.

"Ninawapongeza watangazaji wa kipindi hiki cha MamaMia na uongozi wa East Afrika Radio na EATV kwa kuligusa kundi hili muhimu la wanawake," alisema.

Kitosi alisema katika kipindi cha MamaMia hujadili masuala ya wanawake katika maeneo ya kisiasa, kijamii, kiuchumi na kiuongozi.

"Kundi la wanawake ni muhimu lakini linakabiliwa na matatizo mengi lazima kwa pamoja tushirikiane kuzungumza na kutatua matatizo yao, mbali ya elimu tunayotoa, tumesema hatutaki kubaki ndani ya boksi, tunawafikia wanawake maeneo yao kwa kuandaa makongamano, matamasha, na mafunzo ya kuwainua kiuchumi," alisema.

Kitosi alisema ndipo walioibuka na wazo la kuanzisha kampeni hiyo ya mama lishe ambao kwao wanawaona ni wapambanaji na asilimia kubwa ya watu wanaokwenda kila siku kwenye mizunguko yao hawaachi kula chakula chao kinachopikwa kwa gharama nafuu na kikiwa na ladha.

"Tukasema tuwafikie kupitia wadau, msimu wa kwanza tulianza mwaka jana tukiwa na mdhamini Jaden Home Store, ambaye walitoa vifaa mbalimbali zikiwamo jokofu, brenda, na mixer," alisema.

Alisema katika msimu wa pili wadau mbalimbali wamejitokeza na wamechangia vitu mbalimbali vikiwamo vyakula na vipodozi.

Aliwataja washindi wengine katika msimu huu na maeneo yao ya biashara kwenye mabano ni Lisa Haurelia (Mbezi Makabe) aliyepatiwa brenda, jiko chapchap, unga, sukari, mchele, mafuta ya kupikia na kizimia moto.

"Amina Mvungi (Goba) jiko chapchap, brenda, unga, sukari, mchele, mafuta ya kupikia na kizimia moto.Maryland Junior (Tabata), jiko chapchap, fire blanket, unga, sukari, mchele, mafuta ya kupikia na kizimia moto," alisema. Kitosi aliwataka wengine ni Mariam Kisenga (Temeke Sterio) aliyepewa stand mixer, na jiko la chapchap, unga, sukari, mchele, mafuta ya kupikia na kizimia moto na shera (Kimara) aliyezawadiwa kipashia chakula (Oven), jiko la chapchap, unga, sukari, mchele, mafuta ya kupikia na kizimia moto.

Pia Theopista Stanslaus (Kinondoni B) amepewa brenda, jiko la chapchap, unga, sukari, mchele, mafuta ya kupikia na kizimia moto.

Mshindi wa kwanza, Magreth alisema jirani yake anakofanya biashara ndiye aliyepiga simu wakati kipindi cha MamaMia kikitafuta mamalishe wa msimu huu bila yeye kujua na siku ambayo watangazaji walipotaka kwenda kumtembelea ndipo alipompelekea simu aongee nao kwa ajili ya maandalizi hayo na baada ya kutembelewa ndipo siku mbele akapigiwa simu afike juzi kwenye hafla hiyo bila kujua ni mshindi.

Alisema pikipiki yake ataiingiza kwenye biashara na pia itamsaidia kusambaza chakula kwa sababu amekuwa akipata wateja wa mbali wanaotaka huduma yake.

TANGAZO

WFP

World Food Programme
Programme Alimentaire Mondial
Programa Mundial de Alimentos
برنامج الأغذية العالمي

SAVING LIVES
CHANGING LIVES

# SALE OF USED VEHICLES

The **United Nations World Food Programme** office in Dar es Salaam have used vehicles, Motorcycles, Generators, IT Equipment, office furniture & equipment for sale on an “as-is-where-is” basis to the highest bidder. Prospective buyers will be responsible for payment of duty, VAT and other related charges as established under Government rules and regulations. Only bids with precise prices will be accepted. WFP reserves the right to reject the bid. Bids should be quoted in Tanzanian Shillings.

**All items can be viewed at the following sites below and on the indicated dates and time.**

| Viewing Sites | Date | Time |
|---|---|---|
| WFP Dar es Salaam, Dodoma. Kibondo& Kasulu Office | 24.08.2021 – 26.08.2021 | 0800hrs-1400 hrs |

Sealed bids should be addressed to the **WFP Representative & Country Director, P.O. Box 77778, Plot No. 133 Mwindu Lane Street, Kinondoni, Dar es Salaam and marked “BID FOR PURCHASE OF USED VEHICLE, MOTORCYCLES, EQUIPMENT & FURNITURE 01/2021” and should reach the UNWFP Dar es Salaam Office before Wednesday 03 September 2021. The bids for used vehicles, motorcycles and generators should be enclosed with banker’s cheque amounting 10% of the value of quoted on the bid.** Successful bidder will be required to pay the balance within 7 working days after being notified of their successful bid, failure to which the 10% deposit will be forfeited, and the item will be offered to the next highest bidder.

## USED VEHICLES AND MOTORCYCLES WITH DETAILS FOR DISPOSAL

| LOT | ASSET ID | PLATE No. | Make | Model | Model Code | Inventory No. | Chassis number | Engine Number | Manufacture Year | Odometer (Km) | Location | Status |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | GVLP2740 | T257CD229 | TOYOTA | LANDCRUISER | HZJ76R-RKMRS | 00239428 | JTEEB71J107027744 | 1HZ0814410 | 2015 | 103629 | Dar Es Salaam | Good |
| 2 | GVLP2742 | T257CD232 | TOYOTA | LANDCRUISER | HZJ76R-RKMRS | 00239430 | JTEEB71J707027750 | 1HZ0814430 | 2015 | 93803 | Dar Es Salaam | Good |
| 3 | GVLP2743 | T257CD236 | TOYOTA | LANDCRUISER | HZJ76R-RKMRS | 00239431 | JTEEB71J907027751 | 1HZ0814432 | 2015 | 197191 | Dar Es Salaam | Good |
| 4 | GVLP2744 | T257CD238 | TOYOTA | LANDCRUISER | HZJ76R-RKMRS | 00239432 | JTEEB71J707027778 | 1HZ0814616 | 2015 | 132910 | Dar Es Salaam | Good |
| 5 | GVLP2737 | T257CD227 | TOYOTA | LANDCRUISER | HZJ76R-RKMRS | 00239425 | JTEEB71J807027725 | 1HZ0814242 | 2015 | 156816 | Dar Es Salaam | Good |
| 6 | GVLP2732 | T257CD223 | TOYOTA | LANDCRUISER | HZJ76R-RKMRS | 00239420 | JTEEB71J307027664 | 1HZ0813699 | 2014 | 161917 | Dar Es Salaam | Good |
| 7 | GVLP2032 | T257CD217 | TOYOTA | LANDCRUISER | HZJ76R-RKMRS | 00238720 | JTEEB71J307020164 | 1HZ0744981 | 2013 | 153239 | Dar Es Salaam | Good |
| 8 | | T257CD228 | MOTORCYCLE | HONDA | XL 125 | 00471254 | LTMJD2191F5305976 | JD21E2224640 | 2015 | 14305 | Kasulu | Good |
| 9 | | T257CD235 | MOTORCYCLE | HONDA | XL 125 | 00471232 | LTMJD2199F5306034 | JD21E2224508 | 2015 | 11300 | Kibondo | Good |
| 10 | | T257CD189 | MOTORCYCLE | HONDA | XL 125 | 00694553 | L125S5757553 | L125S5611784 | 2011 | 42247 | Dodoma | Good |
| 11 | | T257CD182 | MOTORCYCLE | HONDA | XL 125 | 00329070 | L125S5757573 | L125S5611716 | 2011 | 48693 | Dar Es Salaam | Good |
| 12 | | T257CD188 | MOTORCYCLE | HONDA | XL 125 | 00694615 | L125S5757638 | L125S5611813 | 2011 | 41740 | Dar Es Salaam | Good |
| 13 | | T257CD185 | MOTORCYCLE | HONDA | XL 125 | 00694614 | L125S5757635 | L125S5611779 | 2011 | 36313 | Dar Es Salaam | Good |

## OFFICE FURNITURE, EQUIPMENT & GENERATORS

| LOT | INVENTORY NO | DESCRIPTION OF ITEM | STATUS | LOCATION |
|---|---|---|---|---|
| | 00885781 | CHEST OF DRAWERS | GOOD | DAR ES SALAAM |
| 14 | 00885588 | MOBILE DRAWER | GOOD | DAR ES SALAAM |
| | 00248108 | CHEST OF DRAWERS | BROKEN | DAR ES SALAAM |
| | 00885590 | FILING CABINET | GOOD | DAR ES SALAAM |
| | 00885589 | FILING CABINET | GOOD | DAR ES SALAAM |
| 15 | 00885624 | FILING CABINET | GOOD | DAR ES SALAAM |
| | 00885626 | CABINET FILE (IRON) | GOOD | DAR ES SALAAM |
| 16 | 00885627 | CABINET FILE (IRON) | GOOD | DAR ES SALAAM |
| | 00885628 | CABINET FILE (IRON) | GOOD | DAR ES SALAAM |
| 17 | 00885629 | FILLING CABINET | GOOD | DAR ES SALAAM |
| | 00169589 | BOOKSHELF | BROKEN | DAR ES SALAAM |
| 18 | 00169591 | BOOKSHELF | BROKEN | DAR ES SALAAM |
| | 00885400 | BOOKSHELF | GOOD | DAR ES SALAAM |
| | 00885481 | SECURITY GUARDS MOBILE HUTS | BROKEN | DAR ES SALAAM |
| 19 | 00885482 | SECURITY GUARDS MOBILE HUTS | BROKEN | DAR ES SALAAM |
| | 00885823 | DESK BEECH 0D302 | GOOD | DAR ES SALAAM |
| 20 | 00169516 | BOOKSHELF LV-HC-180 BEECH | BROKEN | DAR ES SALAAM |
| | 00169518 | BOOKSHELF LV-HC-180 BEECH | BROKEN | DAR ES SALAAM |
| | 00885824 | DESK HOD 5050 | BROKEN | DAR ES SALAAM |
| | 00885829 | DESK | BROKEN | DAR ES SALAAM |
| 21 | 00248087 | FILING CABINET | GOOD | DAR ES SALAAM |
| | 00885587 | DESK | BROKEN | DAR ES SALAAM |
| | 00169750 | PAPER SHREDDING MACHINE | NOT WORKING | DAR ES SALAAM |
| 22 | 00375589 | BOOKSHELF | BROKEN | DAR ES SALAAM |
| 23 | 00537180 | GENERATOR **4.5KW AKSA AAP5500E** | WORKING | DAR ES SALAAM |
| 24 | 00885464 | Water Pump ROBIN | BROKEN | DAR ES SALAAM |
| 25 | 00885567 | GAS ELECTRICAL COOKER OVENER | WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00248363 | TABLE | GOOD | DAR ES SALAAM |
| 26 | 00329276 | AIRCONDITIONER | NOT WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00248261 | AIRCONDITIONER | NOT WORKING | DAR ES SALAAM |
| 27 | 00885467 | AIR CONDITIONER | NOT WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00885661 | AIR CONDITION | NOT WORKING | DAR ES SALAAM |
| 28 | 00329408 | AIR CONDTIONER SANYO | NOT WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00885565 | AIR CONDITIONER LG | NOT WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00885599 | BOOKSHELF | BROKEN | DAR ES SALAAM |
| | 00329889 | WEIGHTING SCALE MACHINE | BROKEN | DAR ES SALAAM |
| | 00329893 | WEIGHTING SCALE MACHINE | BROKEN | DAR ES SALAAM |
| 29 | 00329026 | SCANNER | NOT WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00885871 | WOODEN CUPBOARD | BROKEN | DAR ES SALAAM |
| 30 | 00329917 | GENERATOR OLYMPIAN **20 KVA** | WORKING | DAR ES SALAAM |
| 31 | 00694060 | WATER DISPENSER | WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00329898 | WEIGHTING SCALE MACHINE | BROKEN | DAR ES SALAAM |
| 32 | 00885595 | TELEVISION | NOT WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00375501 | AIR CONDITIONER - WALL MOUNTED | NOT WORKING | DAR ES SALAAM |
| 33 | 00248728 | SCANNER | NOT WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00329311 | AIR CONDITIONER DAIKIN | NOT WORKING | DAR ES SALAAM |
| 34 | 00375063 | WATER DISPENSER | WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00375064 | WATER DISPENSER MP SHED | WORKING | DAR ES SALAAM |
| 35 | 00694091 | DIGITAL WEIGHING SCALE | NOT WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00329295 | MONITOR | WORKING | DAR ES SALAAM |
| 36 | 00471545 | LAPTOP HP ELITEBOOK 850 G2 | WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00329334 | PRINTER | WORKING | DAR ES SALAAM |
| 37 | 00329790 | LAPTOP MACBOOK AIR / PRO | WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00471493 | PHOTOCOPIER KYOCERA | NOT WORKING | DAR ES SALAAM |
| 38 | 00248911 | PRINTER | NOT WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00375678 | PRINTER | NOT WORKING | DAR ES SALAAM |
| 39 | 00248662 | PRINTER | NOT WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00329989 | MONITOR | WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00375645 | MONITOR | WORKING | DAR ES SALAAM |
| 40 | '00329786 | MONITOR - HP COMPAQ FLAT SCREEN | WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00329024 | PRINTER | WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00329164 | MONITOR | WORKING | DAR ES SALAAM |
| 41 | 00885523 | LAPTOP | WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00375643 | MONITOR | WORKING | DAR ES SALAAM |
| 42 | 00471766 | CPU | NOT WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00329176 | MONITOR | WORKING | DAR ES SALAAM |
| 43 | 00471291 | LAPTOP HP ELITEBOOK 850 G2 | WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00471312 | LAPTOP HP ELITEBOOK 850 G2 | WORKING | DAR ES SALAAM |
| 44 | 00329856 | MONITOR | WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00471314 | LAPTOP HP ELITEBOOK 850 G2 | WORKING | DAR ES SALAAM |
| 45 | 00329178 | MONITOR | WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00329912 | MONITOR | WORKING | DAR ES SALAAM |
| 46 | 00169723 | PHOTOCOPIER | WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00375037 | MONITOR | WORKING | DAR ES SALAAM |
| 47 | 00885454 | CPU | WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00471522 | LAPTOP HP ELITEBOOK 850 G2 | WORKING | DAR ES SALAAM |
| 48 | 00471584 | MONITOR | WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00471523 | LAPTOP HP ELITEBOOK 850 G2 | WORKING | DAR ES SALAAM |
| 49 | 00471585 | MONITOR | WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00885445 | LAPTOP HP ELITEBOOK 850 G2 | WORKING | DAR ES SALAAM |
| 50 | 00471586 | MONITOR | WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00471525 | LAPTOP HP ELITEBOOK 850 G2 | WORKING | DAR ES SALAAM |
| 51 | '00471587 | MONITOR | WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00471526 | LAPTOP HP ELITEBOOK 850 G2 | WORKING | DAR ES SALAAM |
| 52 | 00471588 | MONITOR | WORKING | DAR ES SALAAM |
| 53 | 00471589 | MONITOR | WORKING | DAR ES SALAAM |
| 54 | 00471590 | MONITOR | WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00885458 | LAPTOP HP ELITEBOOK 850 G2 | WORKING | DAR ES SALAAM |
| 55 | 00471591 | MONITOR | WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00471546 | LAPTOP HP ELITEBOOK 850 G2 | WORKING | DAR ES SALAAM |
| 56 | 00471570 | MONITOR | WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00537001 | LAPTOP DELL LATITUDE E5470 | WORKING | DAR ES SALAAM |
| 57 | 00471571 | MONITOR | WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00537005 | LAPTOP DELL LATITUDE E5470 | WORKING | DAR ES SALAAM |
| 58 | 00471572 | MONITOR | WORKING | DAR ES SALAAM |
| 59 | 00471573 | MONITOR | WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00537899 | LAPTOP-DELL INSPIRON 5767 | WORKING | DAR ES SALAAM |
| 60 | 00471575 | MONITOR | WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 20008509 | LAPTOP-DELL LATITUDE 7490 | WORKING | DAR ES SALAAM |
| 61 | 00471576 | MONITOR | WORKING | DAR ES SALAAM |
| 62 | 00471577 | MONITOR | WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00471298 | HP Desktop | WORKING | DAR ES SALAAM |
| 63 | 00471578 | MONITOR | WORKING | DAR ES SALAAM |
| 64 | 00471579 | MONITOR | WORKING | DAR ES SALAAM |
| 65 | 00471581 | MONITOR | WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00537002 | LAPTOP DELL LATITUDE E5470 | BROKEN | DAR ES SALAAM |
| 66 | '00471582 | MONITOR | WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00537008 | LAPTOP DELL LATITUDE E5470 | BROKEN | DAR ES SALAAM |
| 67 | 00471583 | MONITOR | WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 20002963 | LAPTOP DELL LATITUDE 7280 | BROKEN | DAR ES SALAAM |
| 68 | 00471592 | MONITOR | WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00537898 | LAPTOP-DELL INSPIRON 5767 | BROKEN | DAR ES SALAAM |
| 69 | 00471593 | MONITOR | WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 20008507 | LAPTOP-DELL LATITUDE 7490 | BROKEN | DAR ES SALAAM |
| 70 | 00471594 | MONITOR | WORKING | DAR ES SALAAM |

# MATANGAZO

WFP

World Food Programme
Programme Alimentaire Mondial
Programa Mundial de Alimentos
برنامج الأغذية العالمي

SAVING LIVES
CHANGING LIVES

## SALE OF USED VEHICLES

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | 00885508 | IPAD 2 64GB | BROKEN | DAR ES SALAAM |
| 71 | 00471596 | MONITOR | WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00885515 | IPAD 2 64GB | BROKEN | DAR ES SALAAM |
| | 00471597 | MONITOR | WORKING | DAR ES SALAAM |
| 72 | 00471600 | MONITOR | WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00471602 | MONITOR | WORKING | DAR ES SALAAM |
| 73 | 00471605 | MONITOR | WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00471606 | MONITOR | WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00471620 | MONITOR | WORKING | DAR ES SALAAM |
| 74 | 00375914 | APC SMART UPS 1500 VA FOR PORT OFFICE | BROKEN | DAR ES SALAAM |
| | 00471629 | MONITOR | WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00375915 | APC SMART UPS 1500 VA FOR PORT OFFICE | BROKEN | DAR ES SALAAM |
| 75 | 00471634 | MONITOR | WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00694221 | UPS - | BROKEN | DAR ES SALAAM |
| | 00471487 | UPS | BROK | DAR ES SALAAM |
| 76 | 00471638 | MONITOR | WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00471299 | DESKTOP | WORKING | DAR ES SALAAM |
| 77 | 00471639 | MONITOR | WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00885514 | UPS APS SMART 1500 | BROKEN | DAR ES SALAAM |
| | 00885893 | PRINTER | BROKEN | DAR ES SALAAM |
| 78 | 00471478 | MONITOR | WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00885675 | DOCKING STATION DELL | BROKEN | DAR ES SALAAM |
| 79 | 00537011 | MONITOR DELL PROFESSIONAL P2016 | WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00885978 | DOCK STATION | BROKEN | DAR ES SALAAM |
| 80 | 00537012 | MONITOR DELL PROFESSIONAL P2016 | WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00537013 | MONITOR DELL PROFESSIONAL P2016 | WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00537014 | MONITOR DELL PROFESSIONAL P2016 | WORKING | DAR ES SALAAM |
| 81 | 00537015 | MONITOR DELL PROFESSIONAL P2016 | WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00537018 | MONITOR DELL PROFESSIONAL P2016 | WORKING | DAR ES SALAAM |
| 82 | 00471491 | MONITOR | WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00537724 | PRINTER ZEBRA BARCODE | WORKING | DAR ES SALAAM |
| 83 | 00537632 | PRINTER-BARCODE | WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00885457 | HP MONITOR | WORKING | DAR ES SALAAM |
| 84 | 00375039 | MONITOR | WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00885472 | MONITOR | BROKEN | DAR ES SALAAM |
| 85 | 00169875 | HP FLAT SCREEN - MONOTOR | BROKEN | DAR ES SALAAM |
| | 00026039 | DELL MONITOR | BROKEN | DAR ES SALAAM |
| 86 | 00329830 | MONITOR LCD WIDE SCREEN | BROKEN | DAR ES SALAAM |
| | 00471756 | MONITOR - MACBOOK APPLE THURNDERBOLT | BROKEN | DAR ES SALAAM |
| 87 | 00885470 | HP MONITOR | BROKEN | DAR ES SALAAM |
| 88 | N/A | BATTERIES 12V | **24 PCS** | DAR ES SALAAM |
| | 00694247 | LAPTOP | NOT WORKING | DAR ES SALAAM |
| 89 | 00885473 | MONITOR | BROKEN | DAR ES SALAAM |
| | 00471350 | LAPTOP | NOT WORKING | DAR ES SALAAM |
| 90 | 00329186 | Monitor | WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00694248 | LAPTOP | NOT WORKING | DAR ES SALAAM |
| 91 | 00537783 | MONITOR | BROKEN | DAR ES SALAAM |
| | 00329983 | LAPTOP | NOT WORKING | DAR ES SALAAM |
| 92 | 00375041 | MONITOR HP | WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00248706 | LAPTOP | NOT WORKING | DAR ES SALAAM |
| | 00375973 | DOCKING STATION | WORKING | KIBONDO |
| 93 | 00471257 | LAPTOP HP ELITEBOOK 850 G2 | WORKING | KIBONDO |
| | 00694671 | MONITOR | WORKING | KIBONDO |
| | 00471258 | LAPTOP HP ELITEBOOK 850 G2 | WORKING | KIBONDO |
| 94 | 00694664 | MONITOR | WORKING | KIBONDO |
| | 00471564 | Laptop (HP) | WORKING | KIBONDO |
| 95 | 00471223 | MONITOR | WORKING | KIBONDO |
| | 00694663 | Laptop (HP EliteBook) | WORKING | KIBONDO |
| 96 | 00375974 | DOCKING STATION | WORKING | KIBONDO |
| | 00471220 | SCANNER HP 5590 | WORKING | KIBONDO |
| 97 | 00471283 | MONITOR | WORKING | KIBONDO |
| | 00471261 | LAPTOP HP ELITEBOOK 850 G2 | NOT WORKING | KIBONDO |
| 98 | 00471613 | MONITOR | WORKING | KIBONDO |
| | 00471262 | LAPTOP HP ELITEBOOK 850 G2 | NOT WORKING | KIBONDO |
| 99 | 00471224 | MONITOR | WORKING | KIBONDO |
| | 00248766 | LAPTOPHP ProBook 6460B | NOT WORKING | KIBONDO |
| 100 | 00329161 | MONITOR | WORKING | KIBONDO |
| 101 | 00471318 | LAPTOP HP ELITEBOOK 850 G2 | NOT WORKING | KIBONDO |

**SPARE PARTS - (Dar Es Salaam)**

| | PART NUMBER | DESCRIPTION | TYPE | QUANTITY |
|---|---|---|---|---|
| | 48510-69365 | UNIT ASSY HEAD LAMP- V8 200 | HEAD LAMP | 2 |
| 102 | 48510-69535 | UNIT ASSY HEAD LAMP- V8 200 | HEAD LAMP | 1 |
| | 750R16 | TUBES | TUBES | 22 |
| 103 | 285/65R17 | TYRE MICHELIN | | 7 |

**CARTRIDGES AND TONERS - (Dar Es Salaam)**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Q2612A | CARTRIDGES HP LASERJET PELIKAN | CARTRIDGES | 3 |
| | Q1338A | CARTRIDGES HP LASER JET 4200 Pelikan | CARTRIDGES | 2 |
| | CB324EE | CARTRIDGES HP PHOTOSMART PREMIUM | CARTRIDGES - for Camera | 5 |
| | CB323EE | CARTRIDGES HP PHOTOSMART PREMIUM | CARTRIDGES - for Camera | 5 |
| | CN684EE | CARTRIDGES HP PHOTOSMART PREMIUM | CARTRIDGES - for Camera | 5 |
| 104 | CB325EE | CARTRIDGES HP PHOTOSMART PREMIUM | CARTRIDGES - for Camera | 5 |
| | TK100 | TONER KYOCERA MITA KM1500 | CARTRIDGES | 2 |
| | C8727AE, BLACK | CARTRIDGES HP DESKJET | CARTRIDGES | 3 |
| | Q3960A | CARTRIDGES HP COLOUR LASERJET 2550-2820-2840 | CARTRIDGES | 4 |
| | C4127A | CARTRIDGES HP LASERJET | CARTRIDGES | 12 |
| | Q6003A | CARTRIDGES HP LASERJET | CARTRIDGES | 1 |
| | C8061A | CARTRIDGES HP LASERJET 4100 | CARTRIDGES | 4 |
| | CANON NPG-1 | TONER CANON NP2020,6320 - DRUM UNIT | CARTRIDGES | 2 |
| | OKI 9PIN | RIBBON CARTRIDGE, OKI | CARTRIDGES | 2 |
| | KX-FA136A | TONER-FAX MACHINE, PANASONIC | TONER | 7 |
| | FSC 26 MFP | TONER Kit Colored FSC 26 MFP TK 590 | TONER | 11 |
| 105 | 1620 - TK 410 | TONER Photocopier 1620 - TK 410 | TONER | 25 |
| | BALL PEN | | BALL PEN | 7313 |

**FURNITURE & EQUIPMENT - (Dar Es Salaam)**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | ALUMINIUM DOOR | | 1 |
| 106 | | OFFICE CHAIR | | 9 |
| | | JUICE MIXER | | 1 |
| 107 | | METAL PIPE | | 1 |
| | | HAND FUEL PUMP BROKEN | | 1 |
| 108 | | FUEL DRUM 200 LTS | | 1 |
| 109 | | FUEL TANK 3000 LTS | | 1 |
| | | RIMS 750X16 FOR L76 LANDCRUISER | | 3 |
| 110 | | BANNERS FROM PI | | 25 |
| 111 | | PLASTIC TABLE | | 5 |
| | | WOODEN PARTITION | | 1 |
| | | METAL BOX | | 1 |
| 112 | | FABRICATED METALS FOR THE SHADE ONE LOT | | 1 |


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KILIMO
WAKALA WA TAIFA WA HIFADHI YA CHAKULA
Kizota Viwandani Area | S.L.P 1050 Dodoma | Simu: +255(0)26 2963953 | Fax:+255(0)26 2963950
Barua pepe: info@nfra.go.tz | Tovuti: www.nfra.go.tz
NFRA

## TANGAZO KWA UMMA

## BEI YA UNUNUZI WA AKIBA YA CHAKULA YA TAIFA MSIMU WA 2021/2022

Serikali kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) hununua nafaka kila mwaka kwa ajili ya akiba ya chakula ya Taifa. Wakala umeanza rasmi ununuzi kwa msimu wa **2021/2022 tarehe 15 Agosti, 2021.** Kwa kuanzia, Wakala umefungua vituo vya ununuzi wa mahindi kwenye kanda zenye uzalishaji mkubwa wa mahindi zinazojumuisha Mikoa ya Ruvuma, Njombe, Songwe, Mbeya, Rukwa na Katavi.

Kutokana na maelekezo ya Serikali, Wizara ya Kilimo kupitia Wakala unanunua mahindi kwa bei ya **shilingi 500** kwa kilo katika vituo vikuu vya Wakala (vituo vyenye ghala kuu za Wakala).

Aidha, bei ya kununulia mahindi katika vituo ambavyo vipo nje ya vituo vikuu itakuwa chini ya shilingi 500 kwa kilo, ambapo Wakala kupitia kanda zinazonunua mahindi utabainisha bei halisi itakayotumika katika vituo husika. Bei hizo zitapangwa kwa kuzingatia umbali kati ya vituo vidogo na vituo vikuu na miundombinu mingine ya usafirishaji wa shehena ya nafaka inayonunuliwa katika vituo vidogo kwenda vituo vikuu.

**Imetolewa na:**
**Afisa Mtendaji Mkuu**
**Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA)**

XXXXXXX

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Klabu kutegemea udhamini Azam, TFF ni kujimaliza kisoka

**KIPENGA** cha Ligi Kuu Tanzania Bara tayari kimepulizwa baada kutangazwa tarehe ya kuanza ligi hiyo, inayotarajiwa kujumuisha timu 16 tofauti na 18 za msimu huu uliomaliza kwa Simba kutwaa ubingwa huo kwa mara ya nne mfululizo.

Kwa sasa timu zinaendelea kujiimarisha kuelekea msimu huo mpya unaotarajiwa kuanza Septemba 29, mwaka huu ikiwa ni siku nne baada ya pazia la ligi hiyo kufunguliwa kwa mechi ya Ngao ya Jamii kati ya Simba na Yanga itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Msimu huu ligi hiyo inatarajiwa kuwa na ushindani mkubwa zaidi kutokana na kuongezeka kwa dau la udhamini baada ya Shirikisho la Soka nchini (TFF) na Kampuni ya Azam Media Limited Mei mwaka huu kuingia mkataba mpya wa haki za matangazo ya televisheni wenye thamani ya Sh. bilioni 225.6 kwa kipindi cha miaka 10.

Ushindani huo unatarajiwa kuongezeka zaidi kwani kwa mujibu wa mkataba huo, zawadi za kifedha kwa mshindi wa kwanza kwenye msimu ujao itakuwa Sh. milioni 500, mshindi wa pili Sh. milioni 250, watatu Sh. milioni 225, mshindi wa nne Sh. milioni 200 na zitakwenda zikipungua hadi timu ya mwisho na zile zitakazocheza mechi ya mtoano zikilamba Sh. milioni 20 kila moja.

Kiasi hicho cha zawadi ni mbali na fedha ambazo zitatolewa kwa kila klabu katika kuzisaidia kwenye masuala ya fedha za usafiri pamoja na mishahara ya wachezaji, jambo ambalo lilikuwa changamoto kubwa kwa baadhi ya klabu kwenye ligi hiyo na kusababisha ushindani kuporomoka.

Kwa ujumla, TFF inastahili pongezi kubwa sana katika kufanikisha udhamini huo, lakini Kampuni ya Azam Media na mshirika mwenza Benki ya KCB ambayo nayo imeingia mkataba wa mwaka mmoja na TFF wa kuwa mdhamini mwenza kwa kutoa Sh. milioni 495.6, baada ya kuona fursa hiyo ya kujitangaza kupitia soka la Tanzania ambalo linazidi kukua kila uchao.

Hata hivyo, huu si wakati wa klabu shiriki kwenye ligi hiyo kubweteka na mkataba huo wa TFF na Azam Media, na badala yake zinapaswa sasa kuingia sokoni kusaka wadhamini wao binafsi kupitia jezi na vifaa vingine vya michezo ili kujiingizia kipato zaidi.


Tunatambua uendesha wa klabu ya soka unahitaji fedha nyingi, hivyo kuishia kuridhika na kiasi kidogo ambacho kitatolewa na wadhamini hao, Azam Media na washirika wake, ni sawa na kujimaliza kisoka kwani hakitatosha kuwalipa vizuri wachezaji ili kuweza kwenda kutoa ushindani Ligi Kuu.

Ni wazi kwa klabu zilizopiga hatua kisoka, mapato yake makubwa hutokana na wadhamini wao binafsi na si wale wanaotafutwa na shirikisho la soka husika, hivyo kuna haja ya wamiliki wa klabu zetu kutoa kipaumbele katika kujitafutia wadhamini wao na si kutegemea hao wa TFF.

Tunaamini kama kila klabu itakuwa na wadhamini wake wakubwa watakaoziwezesha kupata kipato kikubwa mara dufu kuliko mgao watakaopata TFF, kutasaidia kuinua kipato cha wachezaji na zote zitakuwa na msuli mkubwa kuanzia kushindana katika usajili wa wachezaji wenye ubora kama Simba, Yanga na Azam FC, na hatimaye ushindani kuongezeka Ligi Kuu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Shangaa ya Miquissone, Chama, Kisinda uyaone ya Ronaldo, Messi

**CRISTIANO** Ronaldo mwaka 2002, alikuwa kwenye klabu ya Sporting Lisbon ya Ureno. Mwaka 2003 akajiunga na Manchester United ya England na kukipiga hapo hadi mwaka 2009, aliondoka na kwenda kujiunga na Real Madrid ya Hispania. Hapo napo akikaa hadi mwaka 2018, akahama na kwenda kwenye klabu ya Juventus ya Italia.

Mwanasoka mwingine maarufu sana duniani, Lionel Messi, huyu alikuwa kwenye klabu ya Barcelona tangu mwaka 2004 na alidumu hapo kwa miaka yote kiasi kwamba kuna mashabiki walidhani kuwa anaweza kustaafia hapo. Lakini wapi bwana! Mwaka huu, Messi amehama na kwenda kujiunga na klabu ya Paris Saint-Germain.

Kwa mifano hii miwili tu, inaonyesha kuwa hakuna mchezaji yeyote yule duniani atakaa kwenye klabu moja kuanzia ujanani hadi akazeekea hapo. Na kama atakuwapo basi atakuwa ni mchezaji wa kawaida tu asiye na uwezo wowote na msaada kwenye timu. Na hata kama mchezaji huyo yupo, basi kitakachofanyika ni kutemwa tu na klabu yake, akatafute klabu nyingine kwa sababu hana msaada.

Hakuna mchezaji yeyote mzuri ambaye hamezewi mate na klabu nyingine. Na hapo ndipo linapokuja suala ya kuuza wachezaji. Kwa siku za karibuni hapa nchini kumezuka malalamiko na mijadala kwa mashabiki wa soka kutokana na klabu za Simba na Yanga kuuza wachezaji wake.

Imeonekana kama ni kosa kubwa kwa klabu hizo kufanya hivyo. Simba ilimuuza Clatous Chama kwenda klabu ya RS Berkane ya Morocco, pia Luis Miquissone akitajwa kutua klabu ya Al Ahly ya Misri. Klabu ya Yanga nayo ikampiga bei winga wake machachari mwenye mbio kama swala, Tuisila Kisinda kwenda klabu ya RS Berkane.

Hiyo ikasababisha baadhi ya mashabiki kuanza kulaumu ni kwa nini wachezaji hao wameuzwa na ni muhimu kwenye klabu hizo. Tatizo la mashabiki wa soka nchini hasa wa Simba na Yanga, hutaka klabu hizo ziishi kama vile zipo kwenye dunia ya peke yao.

Klabu za Ulaya zikiuza wachezaji wao kutoka huku kwenda kule hata kama ni wachezaji muhimu, wanaona kawaida tu. Lakini Simba na Yanga wakiuza wanaona ajabu na kuibua mijadala ambayo wakati mwingine ukiisoka kwenye mitandao ya kijamii na hata kwenye vipindi mbalimbali vya michezo, unaishia kucheka tu.

Manchester United, Arsenal, Chelsea, Juventus, AS Roma zikiuza mchezaji hata kama ni muhimu ni sawa tu, lakini Simba na Yanga ni nongwa.

Simba na Yanga ni kama klabu zingine tu duniani, zinahitaji kununua wachezaji na kuuza pia. Haiwezekani zenyewe ziwe zinanunua tu. Tena zikinunua wanachama na mashabiki wao wanafurahi kweli kweli. Furaha moyoni na wimbo mdomoni. Ikumbukwe kuwa wanaposajili wanakuwa wanatoka kwenye klabu zingine ambazo nazo pia zina mashabiki. Nao wanaumia pia, lakini wanajua mchezaji wao anakwenda kutafuta maisha na atakuja mwingine.

Vipi kwa klabu hizo inakuwa nongwa? Najua tatizo ni kwamba mashabiki wengi wa soka kwa sasa ni vijana, wanadhani wachezaji wao vipenzi wakiondoka inaweza ikawa ndiyo mwisho wa ubora wa klabu zao. Sivyo hivyo.

Klabu hizi zimeshaondokewa na mamia ya wachezaji na zimebaki kuwa hivyo hivyo na kuzidi kuongezeka ubora na umaarufu kila kukicha. Yanga imeondokewa na wachezaji wengi mno wazuri na huwezi kuwahesabu. Kwa kuwauza, kuondoka wenyewe au kustaafu, lakini imeendelea kuwa vile vile hadi leo hii.

Kwa Simba inatoa mfano tu kuwa miaka michache iliyopita ilikuwa ni kina Juuko Mushid, Emmanuel Okwi na James Kotei ambao walikuwa tegemeo kubwa kwenye klabu hiyo.

Walipoondoka mashabiki hawa hawa walipiga kelele na baadhi kudhani kuwa Simba ingeathirika kwa kushuka kiwango. Wakati huo ndiyo ilikuwa imemsajili Chama ambaye hakuwa na jina kubwa kama ilivyo sasa. Kilichotokea kila mtu anafahamu.

Kwa hiyo, walikuja kina Constantine Kimanda, Nonda Shaaban kwenye klabu ya Yanga wameondoka, lakini hakuna anayewakumbuka tena. Walikuwapo kila William Fuhnbulleh, Damian Kimti, Zamoyoni Mogella, Okwi, Chama, Miquissone, wote wameondoka na watakuja wengine ambao watatamba na wao pia wataondoka.

Hayo ndiyo maisha ya mpira na klabu zote duniani. Hakuna atakayeichezea klabu moja milele.

# Mrema awashangaa wanaopinga chanjo corona

**Na Thobias Mwanakatwe**

MWENYEKITI wa Taifa wa Chama cha Tanzania Labour (TLP), Augustino Mrema, amewataka wananchi kuwapuuza baadhi ya watu wakiwamo wanasiasa wanaopinga chanjo ya corona, akidai kila mtu anawajibika kwa afya yake.

Aidha, amesema kuchanja ni sawa na polisi anapokwambia funga mkanda unapokuwa kwenye gari, anakusaidia ili ukipata ajali usipate madhara zaidi.

Akizungumza jana katika mahojiano nyumbani kwake Sinza jijini Dar es Salaam, alisema kuendelea kuwasikiliza wanaopinga chanjo hiyo ni kupoteza muda, kwani kila mtu anatakiwa kujali afya yake mwenyewe.

Alisema ameshapata chanjo na hawezi huchezea afya yake. Alihoji kuwa watu wote wakiugua corona, mitungi ya gesi ya oksijeni utapatikana wapi na kwamba watafia majumbani.

Mrema alisema siyo mara ya kwanza kwa wananchi wa Tanzania kupata chanjo, lakini inashangaza chanjo hii ya corona imekuwa na upinzani mkali sana, na cha kushangaza miongoni mwa wanaopinga ni viongozi wa kisiasa.

"Kuchanja sawa na polisi anapokwambia funga mkanda unapokuwa kwenye gari, anakusaidia ili hata ukipata ajali huwezi kuumia sana, kwa sababu mkanda utakuzuia," alisema Mrema.

Mrema alisema hofu kwamba waliochanjwa baada ya muda watakuwa mazombi, hizo ni kauli za kuwatia hofu kwani wataalamu waliobobea wa masuala ya afya wameshathibitisha kuwa chanjo hiyo ni salama.

Alisema hakuna sababu ya kuingiwa na hofu katika suala hili, kwani bahati nzuri hata Rais Samia Suluhu Hassan ameonyesha njia kwa kupata chanjo hiyo, ambayo inaendelea kutolewa katika nchi mbalimbali duniani.

Baadhi ya wanasiasa wamekuwa wakiikosoa chanjo hiyo, hivyo kuibua malumbano na baadhi ya viongozi wa serikali.

Mpaka Agosti 14, mwaka huu idadi ya wanaume waliochanjwa ni asilimia 58.3 sawa na 121,002 na 86,389 ni wanawake sawa na asilimia 41.7.

# Miaka 3 jela kuomba rushwa 200,000/- kwa mgonjwa

**Na Jumbe Ismailly,** IGUNGA

MAHAKAMA ya Hakimu Mfawidhi Wilaya ya Igunga, mkoani Tabora imemhukumu muuguzi wa hospitali ya wilaya hiyo, Wallace Kaziri (53), kutumikia kifungo cha miaka mitatu jela au kulipa faini ya Sh. 500,000 baada ya kumtia hatiani kwa makosa ya kuomba na kupokea rushwa ya Sh. 200,000 kwa mgonjwa.

Mwendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Wilaya ya Igunga, Mazengo Joseph, alidai kuwa mshtakiwa huyo alikuwa akikabiliwa na mashtaka matatu ya rushwa.

Mbele ya Hakimu wa Wilaya, Godfrey Rwekit, mwendesha mashtaka alidai shtaka la kwanza la kuomba rushwa, Oktoba 30, mwaka 2019, mshtakiwa akiwa muuguzi wa zamu katika hospitali ya wilaya hiyo, aliomba rushwa ya Sh. 200,000 kutoka kwa Kasemba Bundala, ili aweze kumpatia dawa ya ugonjwa wa kifua kikuu aliyekuwa amelazwa katika hospitali hiyo, Bugumba Luhende, ambaye ni mama wa Bundala.

Pia katika shtaka la pili la kupokea rushwa ya Sh. 50,000, Oktoba 30, 2019, mshtakiwa huyo alipokea kwa njia ya simu ya mkononi Sh. 50,000 kama malipo ya awali ya Sh. 200,000 alizoomba.

Mwendesha mashtaka huyo alidai kwamba katika shtaka la tatu la kupokea rushwa ya Sh. 50,000, Novemba 1, 2019, mshtakiwa alipokea kiasi hicho kama malipo mengine ya awali ya Sh. 200,000 na kufanya jumla ya fedha alizopokea kuwa Sh. 100,000.

Kwa mujibu wa Mazengo mshtakiwa huyo alitenda makosa hayo kinyume na kifungu cha 15 (a) na (2) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11/2007.

Hata hivyo, baada ya kusomewa mashtaka yote, mshtakiwa alikana na upande wa jamhuri ulipopeleka mahakamani jumla ya mashahidi tisa pamoja na vielelezo 12, ushahidi ulimtambua mshtakiwa huyo.

Mwendesha mashtaka huyo alidai kuwa baada ya mahakama kusikiliza ushahidi wa pande zote mbili, Hakimu Rwekiti alisema ushahidi uliotolewa na upande wa Jamhuri umethibitisha bila kuacha shaka yoyote kwamba mshtakiwa ametenda makosa hayo.

Mazengo alisema kwamba kutokana na ushahidi huo mahakama hiyo ilimwona mshtakiwa, Wallace Kaziri, ana hatia na kumhukumu adhabu ya kutumikia kifungo cha miaka mitatu jela au kulipa faini ya Sh. 500,000. Mshtakiwa alifanikiwa kulipa faini hiyo na kuachiwa huru.



Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP), Simon Sirro (kushoto) na Mkurugenzi wa Fedha wa Hoteli ya Ramada Resort by Wyndham, Saleem Aboonhi, wakifungua pazia kuzindua kituo kipya cha Polisi Jangwani Beach, kilichojengwa na hoteli hiyo kwa thamani ya Sh. milioni 25 katika Mtaa wa Kilongawima, Kata ya Kunduchi, mkoani Dar es Salaam juzi. Watatu kulia ni Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, ACP Muliro Jumanne. **PICHA: JOHN BADI**

# EWURA kupunguza masharti uanzishaji vituo vya mafuta

**Na Richard Makore,** MWANZA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (EWURA), inatarajia kuanzisha mpango maalum wa kupunguza masharti ya kuanzisha vituo vya mafuta katika maeneo ya vijijini ili kupunguza tatizo la wananchi kuuza kiholela petroli katika makazi ya watu.

Kadhalika, EWURA imesema hivi sasa haitoi leseni mpya kwa kampuni kubwa ya mafuta mpaka ionyeshe mpango wake wa kujenga vituo vya kuuza mafuta ya petroli na dizeli maeneo ya vijijini.

Meneja wa EWURA Kanda ya Ziwa, George Mhina, aliyasema hayo jana alipozungumza na Nipashe kuhusu mikakati mbalimbali wanayofanya ili kumaliza tatizo la watu kuuza mafuta makazi ya watu hususani vijijini.

Mhina alisema bado kuna tatizo kubwa maeneo ya vijijini kutokana na kutokuwapo vituo vya mafuta na kusababisha wananchi kununua petroli na dizeli vituo holela.

Alisema hilo ni tatizo na kwamba hivi sasa wamepunguza masharti kwa mtu anayetaka kufungua kituo cha mafuta sehemu za vijijini kwa kanda ya ziwa.

Mhina alisema mtu anaweza kufungua kituo cha kawaida ambacho kinagharimu Sh. milioni 50 na hatakiwi kuwa na hati ya kumiliki ardhi katika eneo hilo.

Aliongeza kuwa masharti ya kufungua kituo cha mafuta maeneo ya mijini lazima ardhi iwe na hati na mmiliki anaweza kutumia zaidi ya Sh. milioni 200 kwa ajili ya ujenzi na maandalizi mengine.

"Kwa sasa tuna mpango huo wa kuwahamasisha wananchi wa kawaida kufungua vituo hivyo vijijini na sisi tutahakikisha tunasimamia masuala yote yanayohusu usalama kwa kuwa nishati hiyo ni hatari kuuzwa kiholela bila tahadhari," alisema.

Alisema EWURA inatoa elimu katika maeneo mbalimbali Kanda ya Ziwa kuhusu umuhimu wa watu kufuata sheria za kiusalama ili kujilinda na ajali ya moto.

Aidha, alisema katika kupunguza tatizo la watu kuuza nishati hiyo majumbani, EWURA ina mpango wa kutumia vituo vya mafuta vinavyotembea kupitia kwenye magari maalum.

Kuhusu utoaji wa leseni mpya kwa kampuni kubwa, Mhina alisema sharti la sasa lazima mfanyabiashara aonyeshe mpango wake wa kujenga vituo vya mafuta vijijini.

Aliongeza kuwa utaratibu huo utasaidia wananchi wa vijijini kupata huduma ya kupata petroli na dizeli kwa gharama nafuu na mazingira yenye usalama.

# CCM yaiagiza TAKUKURU kuchunguza ufisadi mil. 50/-

**Na Thobias Mwanakatwe**

KAMATI ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Songwe, imeiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kufanya uchunguzi katika mradi wa ujenzi wa Zahanati ya Kijiji cha Msungwe, wilayani Momba, baada ya kushtukia ufisadi wa Sh. milioni 50.

Kamati hiyo chini ya Mwenyekiti wa CCM Mkoa, Henriko Mkola, ilibaini uwapo wa ubadhirifu wa fedha hizo zilizotolewa na serikali, baada ya kukagua mradi huo.

Mkola baada ya kupokea taarifa ya maendeleo ya ujenzi wa zahanati hiyo iliyotolewa na Kaimu Mhandisi wa Halmashauri ya Wilaya ya Momba, Maria Nsonga, alimtaka Mganga Mkuu wa Wilaya ya Momba, Dk. Benedect Ngaiza, kutoa maelezo kama mkuu wa idara ya afya kama mradi uko sawa.

Katika majibu yake Dk. Ngaiza alisema yeye kama mtaalamu wa idara hiyo anaona ujenzi huo ulikuwa unaendelea sawa na taratibu zimefuatwa.

"Nafikiri kamati iliyoundwa ije ichunguze ili kujiridhishwa, lakini mimi naona kama taratibu zilifuatwa bila shida yeyote, ila kamati na TAKUKURU wao pia watakuja na majibu," alisema Dk. Ngaiza.

Majibu hayo yalionekana kumkera Mwenyekiti wa CCM Mkola na kutoa maagizo kwa TAKUKURU kuanza uchunguzi mara moja kwa kuwa Sh. milioni 50 ni nyingi ukilinganisha na kazi iliyofanyika.

"Fedha hizi ni za wananchi... sisi kama kamati hatujaridhishwa na mradi huu, hivyo Mkuu wa Mkoa unatakiwa kuiagiza TAKUKURU kuanza kazi mara moja, kwani fedha hizi zilitakiwa kukamilisha mradi na wananchi waanze kupata huduma za afya," alisema Mkola.

Aidha, Mkola alimtaka Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Omary Mgumba, kuhakikisha anasimamia mradi huo na kukamilika haraka, ikiwamo kupeleka mganga na muuguzi ili wananchi wa kijiji hicho waanze kupata huduma za afya.

Mkuu wa Wilaya ya Momba, Fackh Lulandala, alisema tayari ofisi yake imeanza kuchukua hatua na kwamba ameagiza wahandisi wote wa halmashauri hiyo kuripoti ofisini kwake.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Mkamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo (kushoto), akishirikiana na wadau akiwamo Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi (katikati) na Mwenyekiti wa Kamati ya Mazingira Taifa, Seif Ali Seif (kulia), kufanya usafi wa mazingira kwenye ufukwe wa Msasani, Mikocheni jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mfumo wakwamisha ununuzi wa dengu

**Na Shaban Njia,** SHINYANGA

MADIWANI wa Halmashauri ya Shinyanga, wameishauri serikali kubadilisha mfumo wa ununuzi wa zao la dengu kutoka katika mfumo wa stakabadhi ghalani na kuwa soko huria, ili kuwanufaisha wakulima wa zao hilo kupata bei nzuri.

Diwani wa Kata ya Ilola, Amos Mshandete, aliyabainisha hayo wakati wa kikao cha baraza la madiwani na kwamba msimu wa kilimo uliopita, baadhi ya vyama vya msingi (Amcos) mpaka sasa havijawalipa wakulima.

Alisema ufumo wa sasa wa stakabadhi ghalani unaonekana hauwanufaishi wakulima wa zao hilo, ambapo Amcos zimekuwa zikinunua kilo moja ya dengu Sh. 900 wakati wafanyabiashara wananunua kwa Sh.1,200 kwa kilo moja.

"Mwenyekiti wa mfumo huu wa stakabadhi ghalani fedha haitoki kwa wakati, jambo ambalo limeleta malalamiko mengi kutoka kwa wakulima wa zao hili katika msimu uliopita, mfumo huru wa soko huria utasaidia kuleta ushindani wa bei," alisema Mshandete.

Naye Diwani wa Didia, Paulo Masele, alisema, msimu uliopita wakati wa ununuzi wa choroko na dengu kwa kutumia mfumo wa stakabadhi ghalani, kuna baadhi ya vyama ya msingi mpaka sasa havijawalipa wakulima fedha zao, jambo ambalo linawakatisha tamaa wakulima kuendelea na mfumo huo.

Akijibu malalamiko hayo, Katibu Tawala wa Wilaya ya Shinyanga, Boniphace Chambi, alisema serikali imekuwa na mpango kabambe wa kuimarisha ushirika, ndio maana kumekuwa na mfumo wa stakabadhi ghalani, ambao unalengo la kumkomboa mkulima.

Aidha, alisema kuwa katika mfumo huo kuna malipo ya kwanza kwa wakulima wanaouza mazao yao katika vyama vya msingi na malipo ya pili yatafuatia baada ya mnada, na kwamba kuuza mazao kwa mfumo wa stakabadhi gharani ni utekelezaji wa ilani ya uchaguzi.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Ngasa Mboje, alisema ni vyema serikali ikasikia kauli za madiwani ambao ni wawakilishi wa wananchi, ambao wamekuwa wakilalamika kuhusu mfumo huo na itasaidia kuongeza ushindani wa bei kati ya Amcos na wafanyabiashara.

# Waziri Jafo aongoza usafi kwenye fukwe Dar

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, ameongoza wadau mbalimbali kufanya usafi wa mazingira kwenye fukwe mkoani Dar es Salaam.

Waziri Jafo jana aliwaomboza wafanyakazi wa Benki ya NBC wakiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo, Theobald, Klabu ya Rotary Dar es Salaam Peninsula pamoja na wakazi wengine wa jiji hilo katika kufanya usafi kwenye ufukwe wa Msasani uliopo Mikocheni.

Akizungumza wakati wa zoezi hilo, Waziri Jafo pamoja na kuwapongeza wadau hao kwa jitihada hizo pia aliagiza manispaa za Kinondoni, Ilala, Temeke na Kigamboni kuhakikisha zinatatua changamoto mbalimbali zinazokabili fukwe zilizoko kwenye manispaa hizo ikiwamo ukosefu wa vyoo.

"Suala la kuboresha huduma muhimu kwenye fukwe zetu si tu kwamba ni jukumu la manispaa husika, bali pia ni mojawapo ya chanzo cha mapato na ajira kwao. Manispaa zinapoboresha huduma hizi muhimu pia hata wananchi watajitokeza kwa wingi kwenye maeneo haya na pia watatumia huduma hizi kwa kuchangia kiasi cha fedha ambazo zitaongeza makusanyo kwa manispaa husika," alisema.

Jafo aliongeza kuwa bado serikali hairidhishwi sana na usafi wa mazingira kwenye fukwe nyingi hususani Dar es Salaam na jitihada za kukabiliana na changamoto hiyo zinaendelea kupitia wataalamu pamoja na wadau mbalimbali wanaoshirikiana na serikali kutatua changamoto hiyo.

"Ndio maana nawapongeza sana Klabu ya Rotary kwa namna wanavyojitoa kushirikiana na serikali kutatua changamoto kama hizi kwa kushirikiana na wadau wengine kama vyuo vya elimu ya juu, kampuni binafsi na taasisi za kifedha ikiwamo Benki ya NBC...huu ni mfano wa kuigwa," alisema.

Kwa upande wake Sabi alisema ushiriki wa benki hiyo kwenye zoezi hilo muhimu ni mwendelezo wa utaratibu wa kawaida wa benki hiyo kujitolea ama msaada au kushiriki moja kwa moja katika shughuli za kijamii ili kujenga ushirikiano kwa jamii wanayoihudumia.

Alisema fukwe hizo zinatumiwa na wananchi mbalimbali ambao pia ni wateja wa benki hiyo hivyo wana kila sababu kusaidia kuboresha usafi wake ili kutoa fursa kwa watumiaji kupumzika katika mazingira safi na salama kwao wakati wakijipumzisha huku wakifikiria mambo muhimu ikiwamo maendeleo ya shughuli zao.

Mwenyekiti wa Kamati ya Mazingira Taifa, Seif Ali Seif, alitoa wito kwa jamii kwa ujumla kuhakikisha kwamba kila mmoja anakuwa askari wa kulinda usafi wa mazingira na uharibu wa miundombinu ya mazingira.

Rais wa Klabu ya Rotary Dar es Salaam Peninsula, Dk. Edmund Issae ambaye klabu yake ndio iliratibu zoezi hilo, alisema wamejipanga kuhakikisha washirikiana vema na wadau muhimu ikiwamo serikali ili kutatua changamoto zinazoikabili jamii ikiwamo suala zima la mazingira.

# Benki sasa zaonyeshwa fursa uvuvi

**Na Beatrice Moses**

BENKI na taasisi za kifedha zimehimizwa kuikopesha mitaji katika miradi ya sekta ya uvuvi ili kuchochea uzalishaji wa mazao ya uvuvi na kuchangia kuinua uchumi.

Akieleza matarajio yake baada ya kutembelea Makao Makuu ya Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, anayeshughulikia uvuvi, Dk. Rashid Tamatama, alisema kuwa sekta ya uvuvi ina nafasi kubwa ya kutengeneza ajira kwa vijana kwani mahitaji ni mkubwa kulinganisha na uzalishaji wa mazao ya uvuvi.

Mahitaji ya mazao ya uvuvi ni tani 750,000 kwa mwaka, lakini mavuno kwa sasa ni tani 483,000 tu. Alisema kuna pengo kubwa kufikia mahitaji na kufafanua kwamba pengo hilo ni fursa kwa taasisi za fedha kuchochea uwekezaji katika sekta hiyo ili kuzalisha ajira.

Alieleza kuwa jiografia ya Tanzania inaruhusu kufanya shughuli za uvuvi kwani ina eneo kubwa la bahari, maziwa na mito. Alisema maeneo hayo yakitumiwa inavyostahili taifa litapiga hatua kubwa ya uzalishaji katika sekta hii na kuifanya itoe mchango mkubwa zaidi katika pato la taifa.

"TADB ndiyo yenye dhamana ya kuendeleza na kukuza sekta za kilimo, mifugo na uvuvi, hivyo benki hii ihamasishe benki nyingine za kibiashara ili mitaji ipatikane na uwekezaji ufanywe kwenye sekta hii," alisema Dk. Tamatama.

Alieleza kuwa changamoto kubwa inayowakabili wavuvi wengi ni upatikanaji wa vifaa vya kufanya uvuvi wa kisasa na endelevu, na kuziomba benki na taasisi za kifedha kuwekeza nguvu kwenye uvuvi ili kuongeza uvunaji wa samaki nchini.

Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Frank Nyabundege, alisema benki yake inaunga mkono juhudi za serikali katika kuendelea sekta ya uvuvi nchini na kwamba ni busara wavuvi wakapewa mikopo ili kukuza uzalishaji.

"Sekta ya uvuvi inaajiri watu wengi. Kuboresha mazingira ya uvuvi kutakuza kipato cha wananchi wengi ambao wanategemea sekta hii," alisema Nyabundege.

Aliongeza kuwa kupitia bajeti ya mwaka 2021/2022 serikali imeitengea TADB fedha kwa lengo la kukuza na kuendelea sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi na kueleza kwamba kwa sababu hiyo benki itaendelea kutekeleza wajibu wake na kuhakikisha sekta ya uvuvi inapata msukumo mpya ili kuongeza uzalishaji.

Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ya mwaka huu wa 2021/2022 inaonyesha kuwa watu 225,000 wameajiriwa na sekta ya uvuvi na watu zaidi ya milioni 4.5 wanapata kipato kupitia shughuli za uvuvi.

# Taasisi za fedha zatakiwa kulegeza masharti mikopo

**Na Gwamaka Alipipi**

TAASISI za kifedha nchini zimetakiwa kuongeza kasi ya utoaji wa mikopo pamoja na kutoa masharti rafiki hususani ya dhamana kwa wakulima wadogo ili kuwapa nafuu wakati huu wa mlipuko wa ugonjwa wa virusi vya corona.

Pendekezo hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki na wadau wa masuala ya kilimo, wabunge pamoja na wataalamu wa masuala ya kifedha wakati wakijadili mabadiliko ya sera ya fedha yaliyofanywa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) katika kupunguza athari za ugonjwa wa virusi vya corona kwenye sekta ya kilimo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Jukwaa Huru la Wadau wa Kilimo (ANSAF), Audax Lukonge, alisema ugonjwa wa virusi vya corona umeathiri sekta ya kilimo kwa kiwango kikubwa, kwamba makundi mbalimbali yameathirika kwa viwango tofauti.

Lukonge alisema kundi kubwa lililoathiriwa na ugonjwa huo ni pamoja na wazalishaji wadogo kwenye kilimo.

"Uzoefu wa ANSAF ni kwamba idadi kubwa ya wahitaji huduma wako ngazi ya uzalilishaji kama wafugaji, wavuvi na wakulima. Maamuzi ya BoT kuleta kichochea uchumi ni mzuri sana kwa wakati huu, hata hivyo suala kubwa ni namna nzuri ya kutafsiri tamko lake kuja kwenye utekelezaji halisi," alisema Lukonge.

Aliongeza: "Ni wakati muafaka kuona benki nyingine zinaleta mikopo mingi ya kutosha. Zaidi sana kuja na masharti rafiki hasa ya dhamana kwa wakopaji wa mwanzo na wadogo."

Profesa Andrew Temu, kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), alisema ugonjwa wa virusi vya corona umeathiri kwa kiwango kikubwa sekta ya kilimo kwamba zaidi ya asilimia 67 ya wakulima wameathirika.

Alisema mazao yaliyokuwa yanasafirishwa kwenda nje ya nchi kama vile kahawa, tumbaku ambayo yalikuwa yanaileteа nchi fedha za kigeni kwa sasa hayasafirishwi tena.

Profesa Temu alisema benki kwa sasa zinapaswa kuchukua nafasi kubwa katika kusaidia kuinua sekta ya kilimo, kwa kuweka dhamana nafuu, riba ndogo.

"Benki zimekuwa zikitoa mikopo kwenye sekta zingine na kuikimbia sekta ya kilimo kutokana na majanga yanayoikumba sekta hiyo, kwa mfano kwa miaka sita iliyopita benki zilikuwa zikitoa mikopo asilimia 16.6 kwa sekta binafsi, asilimia 23 kwa wafanyabiashara, asilimia 11 kwenye kilimo. Lakini kwa miaka ya sasa sekta binafsi imeongezeka hadi asilimia 36, lakini kilimo kimebaki palepale," alisema Profesa Temu.

Mbunge wa Vunjo, Dk. Charles Kimei, alisema: "Asilimia 40 ya mikopo inayokwenda kwenye sekta ya kilimo inatolewa na Benki ya CRDB, hii inaonyesha benki hazijawekeza kwenye kilimo."

Alisema benki zinaogopa kuwekeza kwenye kilimo kutokana na hatari zilizopo kama vile mabadiliko ya tabia nchi, kutokuwapo kwa pembejeo za kutosha.

Mbunge wa Viti Maalum, Neema Lugangira, alisema ugonjwa wa virusi vya corona umeathiri kwa asilimia kubwa biashara ya nchi kwa nchi, hususani mazao ya biashara.

Aliushauri Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) kuongeza uhifadhi wa chakula kutoka tani 500,000 za sasa hadi tani milioni moja, ili kuisaidia nchi kuondokana na baa la njaa miaka ya baadaye.




Mkazi wa Mwanza, Monica Andrew (katikati), akifurahia Power Tiller aliyojishindia wakati wa droo ya tano ya promosheni ya Shinda na Balimi Extra Lager inayoendeshwa na kampuni ya TBL, katika mikoa ya kanda ya ziwa, iliyofanyika Kisesa mwishoni mwa wiki. Kulia ni Mkuu wa Mauzo wa TBL Kanda ya Ziwa, Issa Makani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wazabuni mikoa 18 wanolewa kutumia TANePS

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA) imetoa mafunzo kwa wazabuni kuhusu jinsi ya kushiriki fursa za zabuni za serikali kupitia Mfumo wa Ununuzi kwa Njia ya Mtandao (TANePS).

Akizungumza wakati wa mafunzo yaliyofanyika mkoani Kagera, Ofisa Msimamizi wa Mifumo ya Habari Mkuu, Mapinduzi Muhochi, alisema kuwa mafunzo hayo yametolewa katika mikoa 18 nchini kuanzia Julai hadi Agosti mwaka huu, katika kipindi cha mwezi huu ikiwa ni awamu ya pili, lakini lengo ni kuwafikia wazabuni katika mikoa yote ya Tanzania Bara.

Muhochi alisema kwa kuzingatia mafunzo yaliyotolewa katika mikoa ya Simiyu, Mara, Geita na Kagera ambapo jumla ya washiriki 225 wa mikoa hiyo walipatiwa mafunzo hayo, Mamlaka imeshushudia mwitikio mzuri wa wazabuni wenye nia ya kupata elimu kuhusu jinsi ya kutumia TANePS kwa usahihi.

"Tumeamua kutoa mafunzo haya kwa wazabuni katika mikoa ya Tanzania Bara, ambapo washiriki hawachangii gharama yoyote. Hii ni kutokana na umuhimu wa TANePS na kwa kuzingatia uzoefu tuliopata tangu mfumo huu ulipoanza kufanya kazi," alisema Muhochi.

"Kama tunavyofahamu, hivi sasa michakato yote ya zabuni inafanyika kwa njia ya TANePS. Kwa hiyo, ni muhimu kwa wazabuni kupata uelewa sahihi na wa kutosha wa jinsi ya kutumia mfumo huu kupata fursa za zabuni. Tunashukuru mwitikio ni mzuri na kila mwisho wa mafunzo wazabuni wanasema wamepata uwezo zaidi wa kushiriki kwa ufanisi na wameshuhudia faida za TANePS ukilinganisha na hali ilivyokuwa kabla ya mfumo," aliongeza.

Naye mshiriki wa mafunzo hayo ambaye ni mfanyabiashara wa mjini Bukoba mkoani Kagera, Ibrahim Chikwara, aliishukuru PPRA kwa kutoa mafunzo hayo kwa kuwa yamewaondolea changamoto za uelewa ambazo zilikuwa kikwazo katika kutumia TANePS.

"Kabla ya TANePS tulikuwa tuna changamoto, kwanza kufahamu fursa za zabuni ilibidi ufuatilie sana vyombo vya habari hususan magazeti, usome sana kutafuta fursa za zabuni. Lakini ilipokuja TANePS tukishajisajili tunaingia kwenye mfumo tunaona fursa zote za zabuni," alisema Chikwara.

Alisema awali walipata changamoto ya kutumia mfumo kutokana na kukosa elimu ya kutosha kuhuu mfumo huo, lakini baada ya mafunzo wako tayari kuchangamkia fursa kwa ufasaha kwani wamebaini mianya ya rushwa na kujuana imefungwa.

Awali, wakati wa mafunzo yaliyotolewa mjini Musoma mkoani Mara, mzabuni aliyejikita katika utoaji wa huduma za bidhaa mtambuka, Josephine Marwa, alishukuru PPRA kwa kushirikiana na Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini (GPSA) kutoa elimu ya jinsi ya kutumia TANePS kupata fursa hizo.

Pamoja na mikoa ya Kanda ya Ziwa, mikoa mingine ambayo PPRA imetoa mafunzo kwa kipindi cha mwezi huu ni Tabora, Kigoma, Katavi na Rukwa. Mingine ni Mtwara, Lindi, Ruvuma, Njombe, Songwe, Manyara, Kilimanjaro, Tanga, Pwani na Morogoro.

# Mkumbo aiongezea majukumu TANTRADE

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo, ameitaka Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE) kuwa kituo cha kibiashara kinachotoa taarifa, takwimu sahihi na huduma bora za kibiashara ndani na nje ya nchi ili kukuza na kuendeleza biashara nchini.

Alitoa agizo hilo juzi jijini Dar es Salaam katika hafla ya uzinduzi wa Bodi ya Wakurugenzi ya TANTRADE.

Prof. Mkumbo aliitaka bodi hiyo kusimamia ipasavyo majukumu muhimu ya TANTRADE ikiwamo kuanzisha kanzi data yenye taarifa za kibiashara na kufanya utafiti, ili kujua ni bidhaa gani zinazalishwa kwa wingi nchini.

"Nataka kuona TANTRADE inakuwa kimbilio kwa wanyabiashara katika kuwaunganisha wazalishaji, wasindikaji wafanyabiashara kutoka maeneo ya uzalishaji na walipo wateja wa bidhaa zao ndani na nje ya nchi kwa kutoa taarifa na takwimu sahihi pamoja na huduma bora za kibiashara," alisema Prof. Mkumbo.

Pia, aliitaka bodi hiyo kuhakikisha TANTRADE inaongeza ubunifu katika matumizi ya mifumo mbalimbali ya kimtandao ya biashara inayolenga kuongeza upatikanaji wa taarifa mbalimbali za kibiashara kwa urahisi, ili kuwezesha upatikanaji wa masoko ndani na nje ya nchi kwa bidhaa na huduma zinazozalishwa nchini.

"Bodi hii pia inatakiwa kushirikiana na taasisi mbalimbali pamoja na sekta binafsi katika kuelimisha na kuhamasisha uboreshaji wa bidhaa zinazozalishwa nchini, upatikanaji wa masoko, uendeshaji wa biashara, kujenga uelewa juu ya usafirishaji wa bidhaa hizo kwa wajasiriamali wadogo na wa kati ili kufikia soko la ndani, kikanda na kimataifa," alisema Prof. Mkumbo.

Aidha, aliielekeza bodi hiyo kutekeleza jukumu la msingi la bodi katika kutengeneza mkakati wa kufikia malengo ya taasisi na kusimamia utekelezaji wake kwa kutoa ushauri ndani na nje ya vikao vya bodi.



Waziri wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo (kushoto), akikabidhi tuzo ya kumbukumbu ya Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE), iliyomaliza muda wake kwa aliyekuwa Mkurugenzi wa mamlaka hiyo, Balozi Mteule Edwin Rutageruka, wakati wa hafla ya uzinduzi wa Bodi mpya ya Wakurugenzi ya Mamlaka hiyo, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA**

# Waliokosa masomo kwa ujauzito wapewa fursa

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imetoa fursa kwa wanafunzi waliokatishwa masomo kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo ujauzito kupitia Programu ya Elimu Haina Mwisho inayotolewa kwenye Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi nchini.

Mkuu wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Katumba wilayani ya Rungwe, Mussa Mturuki, aliyasema hayo katika ziara ya waandishi wa habari ya kuangalia miradi mbalimbali ya elimu iliyotekelezwa na serikali iliyoandaliwa na Wizara hiyo.

Alisema kupitia maboresho yaliyofanywa, serikali imeanzisha masomo ya elimu haina mwisho na kupelekea wanafunzi hao kutimiza ndoto ambazo awali zilikatishwa kutokana na sababu za kupata ujauzito, utoro na ugumu wa maisha.

"Mpango huu wa elimu haina mwisho ulianzishwa na Serikali kupitia Wizara ya Elimu ili kumaliza changamoto ya kushindwa kupata elimu iliyokuwa ikiwakabili wanafunzi wa kike ambao wamekuwa wakiacha shule au kufukuzwa kwa sababu mbalimbali ikiwamo ya kupata ujauzito, kukosa sapoti ya mahitaji ya msingi, jambo linalosababisha wengi kuacha shule kwa kuona ni mzigo,"alisema.

Alibainisha kupitia mradi huo, wanafunzi hao wanapata elimu ya sekondari kwa kusoma kidato cha kwanza hadi cha nne kwa miaka miwili, huku pia wakipewa fursa ya kuchagua fani mojawapo ya kusoma.

Alisema mpaka sasa kuna wanafunzi 30 wa elimu haina mwisho ambapo pia wanapata fursa ya watoto wao ya kusoma na kulelewa kwenye vituo hivi vya serikali vinavyotoa elimu ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto.

Akizungumzia ukarabati uliofanyika chuoni hapo, Mturuki alisema wamepokea Sh. milioni 606 kwa ajili ya maboresho ambapo walitumia fedha hizo kujenga majengo mapya na kukarabati ya zamani.

Naye, Mwanafunzi Sada Amani aliishukuru Serikali kwa kufufua ndoto zao hasa baada ya kukaa nyumbani muda mrefu ambapo ameahidi kufanya vizuri kwenye masomo yake ili kufikia ndoto zake.

# Maelfu ya wanafunzi wapata elimu jumuishi

**Na Christina Mwakangale**

ZAIDI ya wanafunzi 100,000 kupitia mradi wa Vodacom Tanzania Foundation (VTF), uitwao E-Fahamu wamenufaika na elimu jumuishi inayoendeshwa kwa teknolojia kwenye madarasa mtandaoni.

Mkurugenzi wa Vodacom Foundation Tanzania Rosalynn Mworia, amesema mradi wa E-Fahamu unalenga kutoa usawa katika upatikanaji wa elimu bora kwa wanafunzi na kuwapatia walimu vifaa stahiki na kujenga upokeaji wa madarasa mtandaoni.

Rosalynn aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam, akisema tovuti zote zenye maudhui ya elimu hiyo hayatozwi gharama kwa watumiaji ili kuwawezesha kufikia shule na vyuo na kwamba lengo ni kuwafikia wanafunzi milioni moja ifikapo mwaka 2025.

"Tunajivunia kupokea heshima kubwa kama hii kutoka serikalini. Heshima hii inaongeza azma yetu kuendelea kushirikiana na serikali kuleta elimu bure kwa wote," alisema Rosalynn.

"E-Fahanu ni jukwaa linalowapatia walimu vifaa vinavyoboresha utoaji wa masomo na kuwapa wanafunzi maudhui, kujifunza kwa kasi, kuelewa vizuri zaidi yanayofundishwa darasani."

Alisema kupitia huduma hiyo, Foundation VTF, inasaidia lengo kuu la Mamlaka ya Elimu ya Tanzania (TEA), kutoa elimu bora iliyoanzishwa mwaka 2001 na kuyafikia malengo ya kielimu ya taifa na kuendeleza kasi ya ufikiaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) hususan namba nne, linalolenga elimu bora.

Aidha, TEA ilitoa cheti cha kutambua mchango endelevu wa Vodacom Tanzania Foundation (VTF) kwa ukuaji wa sekta ya elimu nchini, kutokana na dhamira ya kampuni kutumia mtandao kutimiza ahadi yake ya kutomwacha mtu yeyote nyuma katika elimu kupitia teknolojia.

Mwalimu Damian Mtono kutoka Shule ya Sekondari ya Mtakuja alisema: Nilikuwa napitia vitabu kuandaa namna ya kufundisha wanafunzi wangu, inachukua muda, juhudi nyingi na wengi wetu tumekuwa tukipata wakati mgumu kwa sababu kwanza inabidi kuvipata vitabu vyenyewe ambavyo viko vichache," alisema Mwalimu Damian.

"Instant Schools ilibadilisha kila kitu. Niliweza kupata maudhui kwa haraka na urahisi zaidi kutokana na kutumia mpango huu nimekuwa mwalimu bora wa baiolojia wilayani wanafunzi wangu asilimia 71 wakipasi," aliongezea.

Happiness Juma, mwanafunzi wa shule ya Mtakuja, alisema masomo ya sayansi kwa ujumla yanaonekana kuwa magumu kuelewa, na kwamba yaliyoko kwenye jukwaa la 'Instant Schools' ni rahisi kusoma na kuelewa huku zaidi ya shule 190 zikitumia jukwaa hilo.

# Nipashe Spotika




WAKOKOTAJI MPIRA 10 BORA WA WAKATI WOTE UK. 12 - 13




# 5 BORA YA UPATINA WA USHAMBULIAJI

## ISIKUPITE

KIPA wa Paris Saint-Germain, Keylor Navas ndiye aliyeokoa michomo mingi ya mabao (54) kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita, akifuatiwa na Manuel Neuer wa Bayern Munich (35), Edouard Mendy wa Chelsea (31), Agustin Marchesin wa Porto (29) na Thibaut Courtois wa Real Madri (26).



**LONDON,** England

SOKA ni mchezo wa timu na timu imejengwa juu ya kemia na uelewano kati ya wachezaji. Wakati mwingine mchezaji anaweza kuja ambaye anaweza kuleta ubora kwa wachezaji wenzake. Tumeona mengi.

Luis Suarez-Lionel Messi, Wayne Rooney-Cristiano Ronaldo na Fernando Torres-Steven Gerrard, ni mifano michache ya ushirikiano mzuri wa kushambulia. Katika nyakati za hivi karibuni, tumeona kuibuka kwa 'washikaji' kadhaa wenye ufanisi wa kushambulia.

Lakini ushirikiano wa kushambulia bado ni maarufu sana. Inasikitisha sana kwamba ushirikiano kati ya wachezaji wawili wa kushambulia kutoka msimu wa 2020-21, umevunjwa. Erling Haaland na Jadon Sancho ulikuwa ushirikiano wa kutisha, lakini sasa amejiunga na Manchester United.

Ndivyo ilivyo kwa Romelu Lukaku na Lautaro Martinez. Wawili hao waliongoza katika ushindi wa Inter Milan msimu uliopita, lakini Lukaku sasa amejiunga na Chelsea kwa ada ya euro milioni 115.

Bila kuchelewesha zaidi, wacha tuangalie ushirikiano mzuri wa kushambulia katika mpira wa miguu kwa sasa...

### #5. CRISTIANO RONALDO-FEDERICO CHIESA (JUVENTUS)

Hata akiwa na umri wa miaka 36, Cristiano Ronaldo anaendelea kuwa na nguvu. Anaendelea kutushangaza na mchezo wake wa riadha na uwezo wa kufunga mabao. Ronaldo alishinda Kiatu cha Dhahabu cha Serie A msimu wa 2020-21 baada ya kufunga mabao 29 katika mechi 33.

Licha ya viungo wa Juventus kuwa na msimu mzuri, timu hiyo iliweza kufuzu kwa Ligi ya Mabingwa Ulaya na kushinda pia Coppa Italia. Sifa nyingi kwa hiyo inapaswa kwenda kwa ushirikiano ambao Ronaldo aliweza kuuweka na Federico Chiesa.

Winga wa zamani wa Fiorentina alifunga mabao 15 na kutoa pasi za mwisho 11 katika mechi 46 kwenye mashindano yote ya Juventus. Chiesa amemsaidia Ronaldo vizuri sana na wawili hao wanashiriki uhusiano mzuri kwenye uwanja wa mpira. Inaonekana kama tutaona mpira mzuri zaidi kutoka kwa wawili hao.

### #4. MOHAMED SALAH - SADIO MANE (LIVERPOOL)

Ikiwa tungeweka orodha hii pamoja mwaka mmoja nyuma, wawili hawa wa Liverpool, Mohamed Salah na Sadio Mane wangekuwa juu zaidi kwenye orodha. Lakini, Mane alikuwa na msimu duni wa 2020-21 na bado alionyesha ubora wa kutosha kupata nafasi kwenye orodha hii.

Kabla ya msimu wa 2020-21, Salah na Mane walionekana kuwa hawawezi kuzuiwa. Wawili hao, pamoja na Firmino wa 2020-21, walifanya 'fujo' huko Ulaya na kwenye Ligi Kuu ya England. Ushujaa wao ulikuwa muhimu kwa ushindi wa Liverpool wa Ligi a Mabingwa Ulaya msimu wa 2018-19 na ushindi wao wa Ligi Kuu mwaka 2019-20.

Salah alimaliza wa pili katika mbio za Kiatu cha Dhahabu cha Ligi Kuu msimu wa 2020-21. Alifunga mabao 22 katika mechi 37 za Ligi Kuu. Katika mechi 51 kwenye mashindano yote msimu wa 2020-21, alifunga jumla ya mabao 31.

Mane alifunga mabao 16 na kutoa pasi za mwisho tisa katika mechi 48 kwenye mashindano yote msimu uliopita. Wawili hao walishiriki ushindi wa Kiatu cha Dhahabu cha Ligi Kuu msimu wa 2018-19 na Pierre-Emerick Aubameyang. Wachezaji wote watatu walifunga mabao 22 kila mmoja kwenye ligi msimu huo.

### #3. HARRY KANE-SON HEUNG-MIN (TOTTENHAM HOTSPUR)

Yote yalianza vizuri kwa Tottenham Hotspur katika msimu wa 2020-21. Ilionekana kama mambo yalikuwa yakiingia sawa kwa kikosi cha kocha Jose Mourinho wakati Son na Kane walipoanza Spurs kwa kasi kwenye Ligi Kuu. Wawili hao walishiriki uunganisho wa aina yake uwanjani na walionekana kufunga na kusaidia kujifurahisha.

Lakini kiwango cha wawili hao katikati ya msimu kuliharibu kampeni ya Spurs. Kushoto na upande ambao haukuonyesha sifa za ukombozi, hatimaye Mourinho alifutwa kazi pia. Lakini ushirikiano wa Harry Kane-Son Heun Min uko hapa.

Muingereza huyo alifunga mabao 33 na kutoa pasi za mwisho 17 katika mechi 49 kwenye mashindano yote. Alishinda pia Kiatu cha Dhahabu.

Son alifunga mabao 22 na kutoa pasi za mwisho 17 katika mechi 51 kwenye mashindano yote ya Tottenham Hotspur msimu wa 2020-21. Wanapokuwa kwenye mbio, zao ni kati ya wachezaji wagumu sana kuwadhibiti.

### #2. KYLIAN MBAPPE / LIONEL MESSI-NEYMAR JR. (PARIS SAINT-GERMAIN)

Tumeamua kujumuisha wote watatu kwa sababu hatujui ni yupi atakayependa msimu huu. Inaweza kuwa wote, lakini tunafahamu vizuri ni nini Lionel Messi na Neymar wanaweza kufanya pamoja. Tumeona mengi kule Barcelona.

Kando ya Luis Suarez, Messi na Neymar waliunda bila shaka upatina mkubwa zaidi wa ushambuliaji katika mpira wa kisasa. PSG, watakuwa na waziri mkuu Kylian Mbappe badala ya Suarez. Neymar alikosa sehemu ya msimu wa 2020-21 kutokana na jeraha lake. Bado aliweza kufunga mabao 17 na kutoa pasi za mwisho 11 katika mechi 31 kwenye mashindano yote.

Ushirikiano wake na Mbappe ulikuwa muhimu kwa PSG kuwaua miamba ya Ulaya kama Barcelona na Bayern Munich wakiwa njiani kuelekea nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mbappe alikuwa na msimu bora wa 2020-21. Alifunga mabao 42 na kutoa pasi za mwisho 11 katika mechi 47 kwenye mashindano yote.

### #1. ROBERT LEWANDOWSKI-THOMAS MULLER (BAYERN MUNICH)

Robert Lewandowski bila shaka ni mmoja wa washambuliaji wakubwa wa enzi ya kisasa. Amekuwa hodari sana mbele ya lango katika misimu michache iliyopita na haingekuwa sawa bila mwenzake Thomas Muller.

Muller, anayejiita 'mkalimani' wa nafasi, anacheza kama mshambuliaji wa pili au kiungo mkabaji wa 'Bavaria' hao. Yeye ni mmoja wa wachezaji wenye akili zaidi duniani na harakati zake ni za hali ya juu.

Lewandowski aliifikia rekodi ya Gerd Muller ya mabao mengi zaidi katika msimu mmoja kwa mabao 40 ya Bundesliga kwa kufunga mabao 41 katika mechi 27. Alimaliza msimu akiwa na jumla ya mabao 48 na pasi za mwisho tisa kutoka mechi 40 kwenye mashindano yote.

Wakati huo huo, Muller alifunga mabao 15 na kutoa pasi za mwisho 24 katika mechi 46 kwenye mashindano yote ya Bayern Munich mnamo 2020-21.

# WAKOKOTAJI MPIRA 10 BORA WA WAKATI WOTE


MESSI

**LONDON,** England

VITU vichache sana kwenye mpira wa miguu vinatoa raha kama vile kokota mpira kuliko tekelezwa kikamilifu. Wanasoka ambao wana vipaji na uwezo wa kuwakimbia wapinzani kwa kasi na ujanja wakiwa na mpira mguuni wanapewa sifa sana na kuabudiwa na watazamaji.

**Ni ustadi mgumu, na wachezaji wachache wana uwezo kamili juu ya hili katika kukokota mpira, udhibiti kamili wa mpira unahitajika.**

Makala haya yanawaangalia wachezaji 10 wa wakati wote katika ukokotaji wa mpira duniani, twende sasa...

### #10. ZINEDINE ZIDANE

Mmoja wa wachezaji wakubwa wakati wote na sasa ni mmoja wa makocha bora katika mpira wa miguu duniani, Zinedine Zidane amefanikiwa sana katika soka.

Kipaji kizuri, Zidane alikuwa kiungo wa kifahari, mwenye kipaji cha kitaalamu anayeweza kufanya maajabu mara kwa mara. Mchezaji mbunifu, Zidane alikuwa mmoja wa wanasoka wanaouzwa sana wakati wa ukuu wake, na aliwakilisha klabu kubwa zaidi duniani kama Juventus na Real Madrid.

Mshindi wa Kombe la Dunia na aliwaongoza mara tatu mfululizo Real Madrid kutwaa Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati wa msimu wake wa kwanza klabuni hapo. Alirudi mnamo mwaka 2019, na akashinda taji la LaLiga wakati wa awamu yake ya pili.

### #9. ROBERTO BAGGIO

Roberto Baggio ni mmoja wa wachezaji wakubwa zaidi nchini Italia.

Baggio alianza kucheza soka kule Vicenza, lakini akatengeneza jina lake pale Fiorentina. Kwa kuonekana na wengi kama mmoja wa wachezaji bora zaidi wa klabu, Baggio alipata shida kubwa za kuumia wakati wa kuanza kwa kipindi chake cha Fiorentina.

Juventus walimtaka na Baggio alijiunga na klabu hiyo chini ya mazingira ya kutatanisha. Alishinda Serie A mara moja na 'Kibibi Kizee' hicho cha Turin. Wakati wote wa kazi yake, mchezaji huyo wa kimataifa wa Italia alikuwa maarufu kama mtaalam wa mipira iliokufa na mpiga mkokotaji mpira wa kiwango cha juu dunia, ambaye aliweka ulinzi wa upinzani kwenye miguu yake.

### #8. RONALDO NAZARIO

Mtu huyu anayesifika kwa kubadilisha msimamo wa namba tisa, Ronaldo Nazario, anatajwa kama chanzo cha msukumo na wanasoka wa hali ya juu kama Zlatan Ibrahimovic, Karim Benzema na Kylian Mbappe.

Aliitwa jina la "O Fenomeno", Ronaldo alikuwa mshambuliaji wa kutisha wakati wa uchezaji wake. Nyota wa kimataifa wa Brazil alijumuisha kasi ya haraka na nguvu ya mwili, kudhibiti mpira na akili. Mfungaji bora, Ronaldo anakumbukwa vizuri kwa malengo yake ya kushangaza na chenga za kushangaza.

Ronaldo alishinda Ballon d'Or mara mbili wakati wa uchezaji wake na alishinda Kombe la Dunia mara mbili pia. Lakini mshambuliaji huyu alikuwa na bahati mbaya na majeraha na alipata wakati mbaya ambao ulipunguza kazi yake nzuri.

### #7. RIVELLINO

Rivellino, mkokotaji mpira wa ajabu, alitumia sehemu kubwa ya kazi yake ya kucheza huko Brazil, akiwakilisha klabu za Corinthians na Fluminense wakati huo.

Mchezaji mzuri wa mpira wa miguu, Rivellino alikuwa fundi wa kiwango cha juu duniani ambaye alikuwa hodari wa kuchezewa faulo. Kiungo huyo alikuwa mmoja wa wachezaji muhimu zaidi wa Brazil wakati wakitwaa Kombe la Dunia mwaka 1970.

Rivellino aliondoka Brazil mnamo mwaka 1978 na kuichezea Al-Hilal ya Saudi Arabia. Baada ya misimu michache huko, alistaafu soka mwaka 1981. Alicheza na kustaafu soka katika klabu ya nchini Japan, Shimizu S-Pulse mwaka 1994.

### #6. JOHAN CRUYFF

Bila ushawishi wa Johan Cruyff, kama mchezaji na kama kocha, ni ngumu kufikiria mpira wa miguu ungekuwa wapi leo.

Cruyff alibadilisha mpira wa miguu na mtindo wake wa uchezaji na mchakato wake wa kufikiria. Zao la akademi ya Ajax, Cruyff alikuwa mchezaji bora duniani wakati wa ukuu wake na alikuwa mchezaji mbunifu sana na mfungaji mzuri.

Cruyff aliondoka Ajax mwaka 1973 na kujiunga na Barcelona. Hapa, kwa mara nyingine tena, aliweka urithi wa kudumu. Ajax na Barcelona sasa zimeunganishwa kwa shukrani kwa mtu huyo mkubwa, na alama za vidole za Cruyff bado zinaonekana kwa jinsi klabu zinavyoendeshwa, kutoka chuo cha vijana hadi timu ya wakubwa. Mshindi mara tatu wa Ballon d'Or alifanikiwa Ajax na Barcelona pia, kwa mafanikio makubwa.

### #5. PELE

Kuonekana na wengi kama mchezaji mkubwa aliyecheza mchezo huo, Pele ni moja ya majina yanayotambulika sana katika ulimwengu wa mpira wa miguu.

Mchezaji huyu wa kimataifa wa Brazil alitumia sana kipindi chake cha kucheza katika klabu akiwa na Santos, ambapo ndiye mfungaji bora wa muda wote wa klabu. Lakini, ilikuwa ni kazi yake nzuri Brazil, ambayo ilimpeleka kwa kipindi kirefu. Alishinda Kombe la Dunia mara tatu na timu ya Taifa, na alivutia kila mtu na uwezo wake wa kufunga mabao, ustadi wake wa kupiga chenga na bidii yake.

Pele ndiye mfungaji bora wa muda wote wa Brazil. Mshambuliaji huyo aliondoka Santos mwaka 1974 na kujiunga na New York Cosmos ya Marekani na alistaafu mchezo huo mnamo mwaka 1977.

### #4. RONALDINHO

Brazil ina nia ya kuzalisha vipaji vya kitaalamu, mbele ya ubunifu, na Ronaldinho hakuwa tofauti. Anasifika kwa uwezo wake wa kiwango cha dunia kwenye mpira wa miguu, Ronaldinho alikuwa mchezaji bora zaidi dunia wakati akiwa pale Barcelona. Mchezaji huyu wa kimataifa wa Brazil, alikuwa mjuzi na mjuzi wa hali ya juu, na aliwafanya watu wakae pembeni ya viti vyao kila alipokuwa kwenye mpira.

Ronaldinho alishinda Ballon d'Or mwaka 2005, na alichukua jukumu muhimu katika kumkuza Lionel Messi. Ustadi wa uchezaji wa Ronaldinho na mtindo wake wa uchezaji uliletea shangwe nyingi kwa mashabiki wa mpira kote ulimwenguni.

### #3. LIONEL MESSI

Mtu wa klabu moja, Lionel Messi ni Barcelona. Tangu aanze kuichezea kwa mara ya kwanza mwaka 2004, mchezaji huyu wa kimataifa wa Argentina hajaangalia nyuma, na sasa anachukuliwa kama mchezaji bora zaidi wa klabu moja. Mchezaji wa kiwango cha dunia, muundaji na mfungaji wa mabao, Messi mara nyingi amekuwa tofauti kati ya ushindi wa Barcelona na upotezaji wa Barcelona.

Kwa nchi yake, Messi ndiye anayetengeneza mwonekano bora zaidi na mfungaji bora wa muda wote. Kijana huyu mwenye umri wa miaka 34, hivi karibuni aliongoza nchi yake kutwaa taji la Copa America na sasa ndiye anayeongoza katika mbio za kushinda tuzo yake ya saba ya Ballon d'Or.

### #2. DIEGO MARADONA

Kulikuwa na shinikizo kubwa kwa Maradona kufanikiwa katika soka na aliufanya mpira wa miguu kuonekana rahisi sana kutokana na udhibiti wake wa ajabu.

Maradona alishinda Kombe la Dunia na Argentina mwaka 1986, na akafurahia kazi nzuri kwa kiwango cha juu. Mbali ya uwanja, ingawa alikuwa mtoto kipenzi wa ubishani. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina alikuwa mhusika mkuu wa mafanikio, lakini fikra zake zilikuwa kwamba anachukuliwa kwa heshima kote duniani.

### #1. GARRINCHA

Garrincha alitumia karibu muda wake wote wa uchezaji akiwa Botafogo ya Brazil. Kwa timu ya kitaifa, winga huyo alikuwa kama hirizi. Mpiga chenga wa kiwango cha dunia, Garrincha alishinda Kombe la Dunia mara mbili na Brazil, na alikuwa mchezaji bora kwenye Kombe la Dunia mwaka 1962.

Garrincha alishinda tuzo ya mpira wa dhahabu wa Kombe la Dunia na Kiatu cha Dhahabu cha Kombe la Dunia mwaka 1962. Mshambuliaji huyo alivumilia maisha ya shida nje ya uwanja. Lakini anakumbukwa sana na mashabiki wa mpira wa miguu wa Brazil kwa uwezo wake mzuri wa kupiga chenga. Garrincha bila shaka ni mmoja wa wachezaji wakubwa wa wakati wote wa Brazil.

## Nukuu

"Tunahitaji kuendelea kuimarika na naamini kikosi hiki kinaweza kufanya vizuri zaidi. Tunapaswa kuwa wavumilivu, bado tuna mwezi mmoja wa kujiandaa na nina uhakika timu itakuwa tofauti kabisa baada ya wiki mbili, naiamini timu yangu," **Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes baada ya timu yake kutoka sare ya mabao 2-2 kwenye mechi ya kirafiki dhidi ya FAR Rabat juzi.**



"Nimejaribu kupambana sehemu nyingi, lakini sasa najiona ni mchezaji niliyekamilika zaidi na naamini nitakuwa na wakati bora zaidi hapa. Si kwamba ni mchezaji mpya, nimekuja sehemu ambayo nilikuwapo na nilikwenda sehemu nyingine kwa ajili ya kukamilika, naijua ligi hii na nimefunga mabao mengi hapa," **mshambuliaji wa Chelsea, Romelu Lukaku.**



"Nimeiona Simba yenye mabadiliko kwenye kikosi, wachezaji wenye umri mdogo na wenye morali ya kuipambania timu, kuna mfungaji wa bao la pili (Papa Ousmane Sakho) ni mchezaji bora sana, nadhani atakuwa na mchango mkubwa kwenye timu," **kocha wa zamani wa Simba (kwa sasa FAR Rabat), Sven Vandenbroeck, baada ya timu yake juzi kutoka sare ya mabao 2-2 na Wekundu wa Msimbazi hao.**





# WAJUE WAPINZANI SIMBA, YANGA, MICHUANO CAF

Wapinzani wa Yanga, Rivers United ya Nigeria.
**PICHA: MTANDAO**

**Na Adam Fungamwango**

TANGU Shirikisho la Soka Afrika (CAF), lilipotoa ratiba yake ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho, klabu za Tanzania zipo kwenye maandalizi mazito kujiandaa na mechi hizo.

Simba, Yanga, Azam na Biashara United, ndizo zitakazoiwakilisha nchi kwenye michuano ya kimataifa kwa msimu ujao. Simba na Yanga zitaiwakilisha Tanzania kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, huku Azam na Biashara United zenyewe zitacheza michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Maandalizi kwa timu hizo yanaendelea. Simba na Yanga zimefanya usajili mkubwa, huku timu zote mbili kwa sasa zikiwa nchini Morocco kujiandaa na michuano hiyo.

Azam pia imefanya usajili wa maana, huku leo ikitarajia kuelekea nchini Zambia kuweka kambi kujiandaa na Kombe la Shirikisho.

Biashara United nayo imesajili wachezaji kadhaa. Ni timu ambayo kwa mara ya kwanza itashiriki michuano ya kimataifa, hivyo nayo iko kwenye maandalizi.

Ratiba ya CAF, inaonyesha kuwa Yanga itaanza mechi yake ya Ligi ya Mabingwa nchini Septemba 10 dhidi ya River United ya Nigeria na marudiano ya Septemba 17, mwaka huu.

Simba kutokana na kufanya vizuri kwa miaka ya karibuni kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa, yenyewe imekwenda moja kwa moja kwenye raundi ya kwanza, hivyo itazisubiri timu za Jwaneng Galaxy ya Botswana na Diplomates FC ya Afrika ya Kati zitoane kwanza, ndipo iipokee timu moja kati ya hiyo Oktoba 15 ugenini na Oktoba 22, mwaka huu marudiano nchini Tanzania.

Azam itacheza na Horseed FC ya Somalia Septemba 10 ikianzia nyumbani na marudiano Septemba 17, huku Biashara yenyewe ikianzia ugenini dhidi ya Dikhil FC ya nchini Djibouti.

Kwenye makala haya, tutazitazama timu zote ambazo klabu za Tanzania zitacheza nazo.

### RIVERS UNITED - NIGERIA

Yanga itacheza na timu hii kwenye mechi ya awali ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika. Si timu ya muda mrefu sana. Ilianzishwa mwaka 1916. Ilianzishwa kwa muunganiko wa timu za Sharks FC na Dolphins FC.

Makao makuu ya klabu hii ni Port Harcout nchini Nigeria. Msimu huu imeshika nafasi ya sita kwenye Ligi Kuu nchini Nigeria, ikicheza mechi 38 na kupata pointi 63. Imeshinda mechi 18, sare tisa na imepoteza michezo 11.

Tiketi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika, imeipata kutokana na Ligi Kuu msimu wa 2019/20 iliposhika nafasi ya pili kwa pointi 45 chini ya Plateau ambao ndiyo walitwaa ubingwa.

Hata hivyo, Rivers ilicheza mechi 25 tu na Ligi Kuu ikasimamishwa kutokana na ugonjwa wa Covid-19 na timu mbili za kwanza zikateuliwa kuiwakilisha nchi.

### JWANENG GALAXY - BOTSWANA

Itacheza na Simba kama itafanikiwa kupita kwenye raundi ya awali dhidi ya Diplomates ya Afrika ya Kati. Timu hii ya Botswana, ilianzishwa mwaka 2015 kwa muunganiko wa timu za Jwaneng Comets na Debswana Toungsters.

Timu hiyo imepata tiketi ya kucheza michuano hiyo msimu huu baada ya kuongoza ligi hadi ilipokomaa msimu mmoja uliopita uliopita kutokana na janga la virusi vya corona, ikiwa na pointi 41, ikicheza mechi 20, ikishinda mechi 12, sare tano na kufungwa tatu.

### DIPLOMATES FC - AFRIKA YA KATI

Ni timu ambayo haina historia kubwa sana kwenye soka la Afrika. Ni moja kati ya timu mpya ambazo hazijafanya makubwa sana kwenye soka la Afrika, lakini imesajili wachezaji wazuri na yenye matengemeo ya kuleta upinzani kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika.

Timu hii itacheza na Simba kama itafanikiwa kuitoa Jwaneng Galaxy ya Botswana.

### HORSEED FC - SOMALIA

Hii ni klabu kongwe, iliyoanzishwa mwaka 1971, tofauti na Azam ambayo ilianzishwa mwaka 2004. Makao makuu yake ni Mogadishu. Ndiyo iliyopangwa kucheza na Azam kwenye mechi ya awali ya michuano hiyo.

Ni mabingwa kwenye nchi hiyo ikiwa imecheza mechi 18, ikishinda 11, ikitoka sare tano na kupoteza mechi mbili. Kumbuka kuwa nchi hiyo Ligi Kuu ina timu 10 tu.

### DIKHIL - DJIBOUTI

Inawezekana ikawa ni habari nzuri kwa Biashara United, kwani Dikhil si klabu yenye rekodi nzuri au historia kubwa kwenye soka la Afrika.

Kama Biashara United ikijipanga vema, inaweza kuweka historia nzuri kwa klabu hiyo na soka la Tanzania kwa ujumla.

### JE, WAJUA?



SHIRIKISHO la Soka la Kimataifa (Fifa), limeandika barua kwa serikali kadhaa ambazo mashirikisho yao ni wanachama wake kuomba uhamishaji wa dharura wa wachezaji wa kike kutoka Afghanistan kutokana na kupokea vitisho vya kuuliwa na wanamgambo wa Taliban ambao hawataki kuona wanawake wakicheza mpira.





# Bunge lakataa taarifa ya TAMISEMI

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa imekataa kujadili taarifa ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kuhusu utendaji, utoaji na urejeshaji wa fedha za mikopo ya asilimia 10 ya mapato ya ndani kwenye halmashauri nchini.

Akizungumza sababu za kuikataa taarifa hiyo, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Humphrey Polepole, alisema kamati hiyo haijaridhishwa na taarifa ya Mkoa wa Dar es Salaam ambayo ilitakiwa kuwasilishwa kwa kina ili kusaidia Bunge kuelekeza serikali kwenye utoaji wa mikopo hiyo.

"Ni dhamira njema ya Rais Samia Suluhu Hassan kuhakikisha fedha hizo zinakwenda na ni nyingi mno zaidi ya Sh. bilioni 68, lakini taarifa iliyokuja inashindwa kutusaidia," alisema.

Polepole aliagiza taarifa hiyo iandaliwe vizuri zaidi na kuwasilishwa kwa wakati mwingine kama ratiba itaruhusu.

"Kamati inatoa wito kwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI na kuzielekeza halmashauri zote 184 nchini kuzingatia maelekezo ya serikali ya kutoa fedha za makusanyo ya ndani asilimia 10 kwa ajili ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu, katika kuzisimamia na kuzitoa fedha hizo na kuwe na mchakato wa wazi," alisema.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Ofisi hiyo, David Silinde, aliziagiza halmashuari hizo kutekeleza agizo la kamati na kuhakikisha mchakato wa utoaji wa mikopo unakuwa wa wazi ili watu wote wawe na haki sawa.

"Fedha zinazotakiwa kutolewa zitolewe maana kutotoa mkopo ni kwenda kinyume na kukiuka Sheria ya Bunge na kosa la jinai," alisema.

## Maofisa biashara wapewa jukumu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WIZARA ya Viwanda na Biashara imewataka maofisa biashara kukusanya maoni ya mapitio ya sheria ya leseni za biashara, ili serikali iangalie namna ya kurekebisha ili ikidhi mahitaji ya sasa.

Aidha, imeahidi kuwasilisha malalamiko sehemu husika ya kuchelewa kutolewa kwa vitambulisho vya wajasiriamali.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dotto James, aliyasema hayo juzi alipokuwa akifunga mafunzo ya maofisa biashara kutoka mikoa ya Dodoma, Singida na Morogoro.

"Ni muhimu sana na kama mnaona sheria hii imepitwa na wakati basi nawashauri mkusanye maoni, myachambue na baadaye muyawasilishe serikalini ili kuona namna ya kutatua changamoto hiyo," alisema.

Alibainisha maofisa hao wanadai sheria hiyo imepitwa na wakati na kusababisha kushindwa kufanya kazi kwa ufanisi.

"Nawashauri suala hilo mlifanyie kazi, kakusanyeni maoni myachambue na kuyawasilisha serikalini ili liliweze kufanyiwa kazi," alisema James.

Katibu Mkuu alisema sheria sio msaafu inahuishwa na suala hilo limekuwa likifanyika mara nyingi kama sheria ni ya zamani sana ili kuendana wakati wa sasa.

"Hivi sasa mambo yanaenda yakibadilika kila wakati kulingana na teknolojia kubadilika, hivyo hata sheria hiyo inatakiwa kwenda na wakati na msikae kimya kama mnaona kuna kitu kinamanufaa mnapaswa mkisemee," alisema James.

Akizungumzia ombi la maofisa hao kuiomba wizara hiyo kuwa mlezi wa chama chao ambacho kipo katika hatua za mwisho kukamilika, James alisema wanapaswa kuliandikia hilo kwa kina ikiwamo kuchambua hoja za msingi na kuliwasilisha sehemu husika, ambayo wanaona inafaa kupata mlezi.

"Mnaweza kusema sisi tumekuwa wahanga hatuna mlezi mwenye taaluma yetu tumeona Wizara ya Viwanda na Biashara ambayo ndio inasimamia sheria zote ikiwamo sera na mikakati," alisema James.

"Naomba mhangaikeni na suala hilo na mlipitishe kwa mkurugenzi wa maendeleo ya biashara, ofisi ya Rais TAMISEMI ili kujadiliwa, hata la maofisa biashara kwenda kukusanya ushuru nalo kaeni chini mlijadili," alisema.

Naye katibu wa muda wa Chama cha Maofisa Biashara, Alo Fred, alisema yote aliyowashauri watayafanyia kazi ili kufikia malengo.



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka (katikati), akikata utepe kuashiria kupokea na kukabidhi mabomba ya maji kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa malipo kwa matokeo awamu ya nne, jijini Dodoma mwisho wa wiki. Wengine ni viongozi mbalimbali wa mkoa huo. **PICHA IBRAHIM JOSEPH**

## RUWASA yapewa miezi 3 miradi ya maji

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WAKALA wa Majisafi na Mazingira Vijijini (RUWASA) Mkoa wa Dodoma, umepewa miezi mitatu kuhakikisha unakamilisha ujenzi wa miradi ya maji ili wananchi wapate huduma.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki kwenye hafla ya kupokea mabomba kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa malipo kwa matokea awamu ya nne kimkoa ilifanyika jijini hapa.

Aliutaka wakala huo kuhakikisha unawaunganishia maji wananchi wa maeneo yote yaliyopo kwenye mpango huo ndani ya muda wa miezi mitatu, vinginevyo watawajibishwa kisheria.

"TAKUKURU wapo hapa na Jeshi la Polisi wapo hapa, sisi tumealikwa kwa nia njema kabisa kuja kushuhudia kazi hii nzuri, sasa baada ya miezi mitatu hawa ambao umewakaribisha kuja kushuhudia hafla hii watageuka sasa kuanza kuwashughulikia ninyi kama mkishindwa, sijui kama ninaeleweka," alisema.

Alibainisha kuwa lengo la serikali kutoa vifaa hivyo ni kuondoa tatizo la maji maeneo hayo ambalo limekuwa la muda mrefu, hivyo kutaka nia hiyo isiharibiwe na watendaji wachache wazembe.

Kadhalika, aliutaka wakala huo kuhakikisha vifaa vyote vilivyotolewa kwa ajili ya miradi huo vipelekwa wilaya husika pamoja na vijiji ili kuwafikishia walengwa huduma ya maji kwa haraka.

Naye, Mbunge wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, alisema kuna baadhi ya miradi iliyokuwa ikitekelezwa na Wizara ya Maji kupitia mradi wa DDCA haikufanya vizuri na haikukamilishwa kwenye jimbo lake.

Alisema kuna miradi 13 ya maji ambayo inatekelezwa, lakini kuna baadhi imekwama kutokana na rasilimali fedha.

Mavunde alitaja tatizo lingine ni mradi wa maji Kijiji cha Chididimo kumezwa na maji ya bwawa kutokana na kujengwa karibu na bwawa jambo ambalo limesababisha wananchi kukosa huduma hiyo.

Awali, akitoa maelezo ya utekelezaji wa mradi huo, Meneja wa RUWASA Mkoa wa Dodoma, Dk. Godfrey Mbabaye, alisema mabomba hayo yana urefu wa mita 35,232 yenye vipenyo mbalimbali.

Dk. Mbabaye alisema mabomba hayo yatagawiwa katika wilaya zote saba za mkoa wa huo ambapo Kongwa itapata mita 7,100, Bahi mita 600, Chemba mita 2,550, Mpwapwa mita 4,691, Kondoa mita 7,500, Chwamwino mita 5,581na Dodoma Jiji mita 7,210.

Aidha, alisema mpango huo utarejesha huduma ya maji katika vituo 2,059 visivyotoa huduma hiyo katika wilaya hizo na utawanufaisha wananchi 1,324,255 sawa na asilimia 61.9 ya wakazi 2,139,450 waishio maeneo ya vijijini katika mkoa huo.



# Marekani yaipiga jeki Tanzania huduma afya

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

SERIKALI ya Marekani kupitia Taasisi yake ya Utafiti ya Jeshi ya Walter Reed imeikabidhi Serikali ya Tanzania vituo viwili vya kutolea huduma na matibabu kwa watu wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (VVU) katika mikoa miwili ya Nyanda za Juu Kusini.

Vituo hivyo vitasaidia kuongeza mapambano dhidi ya maambukizi mapya ya virusi hivyo.

Aidha, imeikabidhi kliniki moja ya afya ya uzazi na afya ya mtoto ili kuwasaidia wananchi kupata huduma bora za afya ya uzazi na matibabu sahihi kwa watoto ili kupunguza vifo vya watoto wachanga nchini.

Mikoa iliyonufaika na msaada huo ni Mbeya na Songwe ambapo Mbeya imepata kituo kimoja cha kutolea huduma na matibabu kwa watu wanaoishi na VVU na kliniki ya afya ya uzazi na afya ya mtoto, huku Mkoa wa Songwe ukipata kituo cha matibabu kwa watu wanaoishi na VVU.

Katika Mkoa wa Mbeya, kituo cha huduma na matibabu kwa watu wanaoishi na VVU kimejengwa katika hospitali inayomilikiwa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Konde kilichopo Matema wilayani Kyela na kliniki ya afya ya uzazi na afya ya mtoto kimejengwa katika kituo cha afya cha Ipinda wilayani Kyela. Katika Mkoa wa Songwe kituo cha huduma na matibabu kwa watu wanaoishi na maambukizi ya VVU kimejengwa katika Hospitali ya Mwambani wilayani Songwe.

Balozi wa Marekani nchini, Donald Wright, alikabidhi vituo hivyo kwa pamoja mwishoni mwa wiki katika hafla iliyofanyikia kwenye Hospitali ya Lutheran Matema wilayani Kyela, ambapo alisema msaada huo ni sehemu ya malengo ya Serikali ya Marekani kusaidiana na Tanzania kuboresha maisha ya wananchi.

"Tanzania na Marekani tumekuwa na ushirikiano kwa zaidi ya miaka 60 sasa, hivyo mwaka huu wakati mtakapokuwa mnasherehekea miaka 60 ya Uhuru nasi tutashirikiana nayi kusherehekea ushirikiano wetu, hivyo msaada wa vituo hivi ni sehemu ya kuimarisha ushirikiano huu," alisema Balozi Wright.

Alisema wataendelea kushirikiana na serikali pamoja na wadau wengine kuhakikisha huduma bora za kiafya zinawafikia Watanzania wote bila kubaguliwa kwa namna yoyote.

Mkurugenzi wa Walter Reed Tanzania, Mark Breda, alisema alisema vituo hivyo vitawasaidia watu wanaoishi na VVU kupata huduma kwenye maeneo yenye nafasi ya kutosha, faragha zaidi na huduma zilizoboreshwa.

Alisema vituo hivyo vitasaidia pia kukabiliana na maambukizi ya VVU kwa maelezo kuwa wananchi watapata ushauri na elimu ya VVU bila kuogopa kutokana na kutolewa kwenye maeneo ya siri.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ukimwi, Kifua Kikuu, Dawa za Kulevya na Magonjwa yasiyo ya kuambukizwa, Fatuma Taufiki, aliomba huduma za Shirika la Walter Reed zisambae maeneo mengi zaidi nchini.

"Shirika hili linafanya kazi nzuri sana, lakini tunaomba hizi huduma zisambae na katika mikoa mingine, tunajua hii mikoa ya Nyanda za Juu Kusini maambukizi ni makubwa lakini hata mikoa mingine tunaamini tabia zinafanana hivyo nayo ifikiwe," alisema Taufiki.

Akipokea vituo hivyo kwa niaba ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Ismail Mlawa, aliishukuru Serikali ya Marekani kwa msaada huo huku akiwataka Watanzania kujipanga kujitegemea.



Baadhi ya vijana wakipakia madawati kwenye gari yanayodaiwa kununuliwa na Halmashauri ya Jiji la Mbeya, katika eneo la Sokoine, jijini Mbeya mwishoni mwa wiki, kwa ajili ya kukabiliana na tatizo la uhaba wa samani hizo kwenye shule za msingi na sekondari. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## DC apiga 'stop' watoto maeneo ya machimbo

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

MKUU wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, amepiga marufuku watoto wenye umri wa chini ya miaka 18 kuonekana kwenye maeneo yote yanayojihusisha na shughuli za uchimaji wa madini.

Aidha, alisema atawachukulia hatua za kisheria watakaobainika kuwatumikisha watoto.

Mfune aliyasema hayo kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika katika kata za Mapogoro na Lugelele yaliko machimbo ya dhahabu, ambapo alisema maeneo hayo siyo salama kwa watoto na ni kinyume kwa mujibu wa sheria kuwatumikisha watoto.

Vilevile, aliwataka wananchi wanaofanya kazi kwenye maeneo hayo kuhakikisha wanafuata taratibu zote za usalama ili kuepuka madhara yanayoweza kuwakuta, endapo hawatachukua tahadhari ikiwamo migodi hiyo kuporomoka na kuwadhuru.

"Marufuku kuleta watoto kwenye maeneo ya machimbo, tukija tena na tukakuta watoto huku, utakachokipata utasimulia, kwanza hairuhusiwi kuajiri watoto wadogo, ukimleta mtoto hapa unamweka kwenye mazingira hatarishi," alisema Mfune.

Alisema kwa wale wenye watoto wanatakiwa kuwaacha watoto nyumbani wanapoenda kwenye machimbo na kwa wale watoto wenye umri wa kwenda shuleni wanatakiwa wawe shuleni na sio vinginevyo.

Alisema walienda katika eneo hilo kwa lengo la kutoa elimu, lakini hatua zitaanza kuchukuliwa watakapobaini kuwa vitendo hivyo vinaendelea kufanyika.

# Mbeya yapewa bil. 1/- ujenzi wa vituo afya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKOA wa Mbeya umepokea Sh. bilioni moja kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya vya kata ambazo zinapatikana kwenye tarafa ambazo hazijawahi kuwa na vituo hivyo, ili kuwapunguzia wananchi adha ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma za afya.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliyasema hayo juzi alipokuwa anawasilisha taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwenye kikao cha Kamati ya Siasa ya chama hicho Mkoa kilichofanyika jijini Mbeya.

Alisema fedha hizo zimetokana na makato ya miamala ya simu ambayo yalianza hivi karibuni, na kwamba pamoja na kwamba makato hayo yamekuwa yakitafsiriwa na baadhi ya watanzania kuwa yana maumivu, lakini yameanza kuleta matunda.

Alisema vituo hivyo vitajengwa katika Halmashauri nne za Mkoa huo ambazo ni Kyela, Chunya, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya na Jiji la Mbeya na kwamba kila Halmashauri itapatiwa Sh. milioni 250 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa vituo hivyo.

"Kwa mara ya kwanza Tarafa ya Unyakyusa wilayani Kyela na Tarafa ya Kipembawe wilayani Chunya zinaenda kupata vituo vya afya, kwa hiyo nawaomba Watanzania tuvumilie na tukubali kukatwa, maana matunda yake yanaonekana," alisema Homera. Alisema hata yeye pamoja na viongozi wengine wa serikali wanakatwa makato hayo, hivyo aliwataka wananchi wa Mkoa wa Mbeya kuendelea kuwa wazalendo kwa kukubali kukatwa fedha hizo ili zilete maendeleo.

Homera alisema mbali na ujenzi wa vituo vya afya katika Mkoa huo, pia Serikali imefanya mambo makubwa kwenye ujenzi wa miundombinu ya elimu, maji na barabara vitu ambavyo alisema vinawasaidia wananchi kupata maendeleo.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mbeya, Mchungaji Jacob Mwakasole, aliipongeza serikali kwa kutekeleza vizuri vipaombele vya ilani ya uchaguzi na kwamba chama hicho kimeridhika na kitaendelea kuisimamia serikali.

Alisema katika Kamati ya Siasa ya Chama hicho imezunguka katika wilaya zote za Mkoa huo kwa ajili ya kukagua utekelezaji wa Ilani na imejiridhisha kwamba miradi inatekelezwa ipasavyo huku wananchi pia wakishiriki.

Alisema kinachotatanisha kwenye tozo za kwenye miamala ya simu ni wananchi kukosa elimu ya kutosha kabla ya kuanza kutumika na kwamba ndiyo sababu iliyowafanya Watanzania waone kama wanaibiwa.

Alisema endapo Watanzania wangeelimishwa vizuri hakuna hata mmoja ambaye angepinga jambo hilo la kimaendeleo, hivyo aliwaomba Watanzania kuendelea kuwa wavumilivu wakati serikali ikiendelea na michakato ya kuboresha.

Meneja wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Mbeya, Matrida Kunenge, alisema katika Mwaka wa Fedha wa 2020/2021, mkoa huo ulikusanya Sh. bilioni 70 kati ya Sh. bilioni 74 walizokuwa wamepanga kukusanya.

# Watumishi matatani kwa tuhuma za utapeli

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WATUMISHI wawili wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali wanashikiliwa na Jeshi la Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi kwa tuhuma za utapeli.

Kamanda wa Polisi Mkoa huo, Awadh Juma Haji, aliwataja watuhumiwa hao ni Biubwa Sudi Mohammed (48), mkazi wa Mwera ( mwalimu wa Shule ya Msingi Fuoni) na Haji Ali Amour (45) mkazi wa Kisauni ambaye ni Ofisa Takwimu Idara ya Elimu Wilaya ya Mjini Unguja.

Alisema watuhumiwa ni watatu, lakini mmoja wao, Ali Khamis Rashid (42) mkazi wa Tomondo alikuwa mtumishi wa serikali, lakini alishafukuzwa kazi kwa tuhuma za utapeli.

Aidha alisema watuhumiwa wanatuhumiwa kwa kosa la kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu, na kwamba Julai mwaka 2020 katika siku tofauti na maeneo tofauti ya Mkoa wa Mjini Magharibi, walijipatia fedha kwa njia ya udanganyifu kutoka kwa watu 20.

Kamanda Awadh, alisema watuhumiwa hao waliwalaghai watu hao kuwasaidia kupata ajira serikalini katika kazi ya ualimu na uhudumu ifikapo Septemba mwaka jana.

Alisema waliwataka kila mmoja kutoa Sh.1,000,000 na kufanikiwa kujipatia fedha Sh. 19,000,000.

"Watuhumiwa hawa ilipofika Septemba mwaka jana waliendelea kuwadanganya kuendea kuwa na subira mpaka utakapomalizika uchaguzi mkuu wa Oktoba na baada ya uchaguzi kumalizika wakaendelea kuwalaghai na baadaye walibaini kuwa wametapeliwa ndipo walipofika polisi kuripoti," alisema Kamanda Awadhi.

Alieleza kuwa watuhumiwa wapo chini ya ulinzi na upelelezi utakapokamilika watafikishwa mahakamani.

Hata hivyo aliwataka wananchi kuwa makini na watu wanaotumia mbinu mbalimbali za kiutapeli kwa kuwalaghai kuwa watawasaidia kupata ajira na badala yake kutoa taarifa katika kituo cha polisi ili kukamatwa mara moja.

Pia Kamanda Awadh alisema jeshi hilo linawashikilia watu 10 ambao ni miongoni mwa wahalifu wanaojishughulisha na vitendo mbalimbali vya uhalifu ikiwamo wizi.

Alisema watuhumiwa hao wlikamatwa Agosti 11 mwaka huu majira ya asubuhi maeneo ya Ziwatuwe na Mboriborini Wilaya ya Mjini Unguja katika muendelezo wa operesheni yao ya kubambana na uhalifu.

Aliwataja ni Sadamu Khamis Makame (25), Mkaazi wa Kilimahewa Bondeni, Husein Ali Ninamia (22), Amour Zahor Said (22), wote wakazi wa Ziwatuwe, Hassani Rashid Ame (18), Mohamed Hussein Mohamed (18) na Ibrahim Hamadi Kitunda (19) wakazi wa Mikunguni.

Wengine ni Ramadhani Kombo Juma (35) mkazi wa Kwahani, Abdalla Juma Abdalla (35), mkazi wa Amani, Mtumwa Khamis Faki (26), mkazi wa Shaurimoyo na Ibrahimu Salum Juma (25) mkazi wa Kwamtipura.

Aidha alisema watuhumiwa hao wanatoka maeneo tofauti na walikuwa wanakwenda katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya kufanya uhalifu ikiwamo kupiga watu mapanga, wizi, uvunjaji na kuwa kero kwa wananchi wa maeneo hayo.

Alielezea watafikishwa mahakamani upelelezi utakapokamilika.



Muuzaji wa viungo akionyesha bidhaa zake kwa watalii katika eneo la Darajani, Mjini Unguja jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Jamii yatakiwa kuelewa umuhimu uongozi bora

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Jumuiya ya Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA), Jamila Mahmoud Juma, amesema ipo haja kwa jamii kufahamu umuhimu wa uongozi bora na demokrasia katika maeneo yao wanayoishi ili kujenga jamii yenye usawa. Aliyasema hayo Mjini Zanzibar wakati akifungua mafunzo ya siku tatu kwa vijana 60 kutoka wilaya zote za Unguja, ambao watakuwa na kazi ya uhamasishaji katika jamii kuhusu umuhimu wa wanawake kushiriki kwenye uongozi na demokrasia.

Alisema vijana watakuwa na kazi ya kuwaelimisha wengine kwenye jamii sambamba na kuhamasisha wanawake kushiriki kwenye nafasi za uongozi.

Alieleza kuwa kupitia elimu hiyo, anaamini wanawake wengi watajitokeza kuwania nafasi za uongozi au hata kuhakikisha wanachagua viongozi wazuri na wenye manufaa kwa maslahi yao.

Baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo walisema mafunzo hayo yamekuja wakati mwafaka na wanaamini watayafanyia kazi.

Fransiska Camilius Clement, alisema uwapo wa nafasi maalum za uongozi kwa wanawake ni kitu ambacho hakipaswi kuondolewa kwa kuwa kunatoa fursa kwa wanawake wengi kujiadaa.

Naye Mratibu wa mradi wa ushirikishaji wanawake katika uongozi kutoka Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), ofisi ya Zanzibar, Salma Amir Lusangi, alisema mradi huo unalenga kuwafikia wanawake 6,000 ili kudai haki zao katika uongozi.

Aliwataka washiriki wa mafunzo hayo waelewe kwamba wana jukumu kubwa la kuwahamasisha wanawake kudai haki zao za uongozi, zikiwamo za kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Alisema kuna haja ya jamii kuwaunga mkono wanawake wanaojitokeza kugombea nafasi mbalimbali za uongozi, kwa sababu ni watu waliojaaliwa huruma kuliko wanaume, hivyo ni rahisi kutekeleza majukumu yao.

# 'Sekta ya sheria ni muhimu kwa haki za binadamu'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MRATIBU wa Kitaifa wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), Onesmo Olengurumwa, alisema sekta ya sheria ni pana na ina mchango mkubwa katika kutetea haki za wananchi.

Akizungumza juzi wakati akifunga mafunzo ya mawakili na wanasheria Mjini Zanzibar yaliyoandaliwa na THRDC, Olengurumwa alisema kuna baadhi ya kesi zinahitaji kufanyiwa kazi kubwa na mawakili wanapaswa kuzisimamia hasa ambazo zinajumuisha watu wengi katika masuala ya haki za binadamu.

Alisema njia za kwenda mahakamani zinazotumiwa na mawakili zikitumika vizuri, wananchi watapunguza kwa kiasi kikubwa kudai haki zao kwa kuandamana.

Naye Meneja Programu wa American Bar Association Rule of Law Initiatives, Afrika Mashariki, Violah Ajok, alisema amefurahishwa kufika Zanzibar na kushuhudia mawakili wenye uwezo mkubwa kuhusiana na kuendesha kesi zenye maslahi kwa umma, huku akiwahimiza kuendelea kujifunza ili kuitumikia jamii katika kujua na kutetea haki zao.

Rais wa Chama cha Wanasheria Zanzibar (ZLS), Hassan Kijogoo, alisema kwa Zanzibar mawakili wanaoshughulikia kesi za umma ni wachache sana, hivyo mafunzo hayo yataongea wingi wa mawakili kwa kuwa wananchi wameanza kujua haki zao na kuzidai kupitia mahakama.

Mwakilishi wa Kituo cha Huduma na Sheria Zanzibar (ZLSC), Jamila Masoud Khamis, alisema mafunzo hayo kwa mawakili yatasaidia kuwapa nguvu na ujasiri katika upatikanaji wa haki zenye za wananchi.

Mawakili na wanasheria walipatiwa mafunzo hayo, walisema yatasaidia kuwajengea uwezo kwa sababu wana kazi kubwa ya kwenda kuwawakilisha wananchi mahakamani katika kesi zenye mtazamo wa kuwajumuisha watu wengi katika jamii.

Zahran Muhammed Yussuf, Wakili wa Mahakama Kuu Zanzibar, alisema mafunzo hayo yamewafikia muda mwafaka kwa sababu kipindi hiki haki nyingi za binadamu zinavunjwa na waovunja ni kwa maslahi yao bila kuangalia athari kwa jamii.

# Wananchi watakiwa kuhoji matumizi ya kodi zao

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, Anderson Msumba, amewataka wananchi kulipa kodi kwa wakati pamoja na kuhoji matumizi ya fedha zao zinazotengwa kwa shughuli za maendeleo.

Msumba aliyabainisha hayo jana wakati akizungumza na vyombo vya habari kuwa wananchi wanatakiwa kuwa huru na kuhoji kodi zao zinavyotumika ikiwamo kwenye sekta ya afya, elimu, kilimo na miundombinu ya barabara.

Alisema kwa sasa wameanzisha utaratibu wa kubandika kwenye mbao za matangazo mapato yanayokusanywa kila mwezi kwa kata 20 zinazounda halmashauri hiyo lengo likiwa ni kwa kila mwananchi aweze kuona kiasi gani kilichokusanywa na kilichotumika ili kuondoa maneno.

Aidha, Msumba alisema mwaka wa fedha uliopita walipanga kukusanya Sh. bilioni 8.9, lakini walivuka lengo na kukusanya Sh. biilioni 9.6.

Alisema moja ya sababu ya kufanya vizuri kwenye mapato ni ushuru wa huduma kutoka mgodi wa Barrick Buzwagi.

"Utaratibu tulioanzisha kwa sasa ni kubandika kwenye mbao za matangazo zilizopo kwenye kata zetu na hapa ofisini kwangu kiasi tulichokusanya na tulichotumia, lengo letu tunataka wananchi watambue kile wanachotoa kinatumika vipi," alisema Msumba.



Mwanasheria wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), Mkoa wa Dar es Salaam, Bonaventure Mwambaja (kushoto), akimsikiliza mmoja wa wanafunzi wa Shule ya Msingi Joyland akielezea kuhusu namna ya kuzalisha umeme kwa kutumia upepo, wakati wa mahafali ya shule ya awali, msingi na sekondari ya Joyland, eneo la Toangoma Kigamboni, mkoani Dar es Salaam. Kushoto kwake ni Mkurugenzi wa shule hiyo, Fredrick Otieno. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# NMB yawakopesha vijana bajaji, bodaboda

**Na Mwandishi Wetu**

VIJANA wa mikoa ya kusini wamewezeshwa kwa kupatiwa mikopo ya bajaji na bodaboba.

Uwezeshaji huo umefanywa na Benki ya NMB Kanda ya Kusini kwa kuzindua huduma ya mikopo ya pikipiki ya miguu miwili na mitatu maalum kwa vijana wanaojishughulisha na usafirishaji wa abiria kupitia vyombo hivyo vya usafiri katika mikoa ya Mtwara, Ruvuma na Lindi.

Huduma hiyo ijulikanayo kama 'NMB master loan', ilizinduliwa mkoani Mtwara na Katibu Tawala wa Mkoa huo, Abdallaha Malela, kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa, Brigadia Jeneral Marco Gaguti.

Mkoa wa Mtwara unakuwa mkoa wa sita kuzindua hiyo huduma ya 'NMB master loan' baada ya kuzinduliwa katika mkoa wa Dar es Salaam na kupelekwa katika mikoa mingine.

Akizungumza wakati wa hafla ya uzinduzi, Meneja wa NMB Kanda ya Kusini, Janet Shango, alisema uzinduzi wa mikopo hiyo ni utekelezaji wa maelezo ya serikali yaliyotolewa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bimge, Ajira, Vijana na Watu wenye ulemavu), Jenista Mhagama, Oktoba mwaka 2019.

"Wakati tunazindua mfumo wa NMB Mastercard serikali ilitupa changamoto hiyo ya kuhakikisha kwamba tunatekeleza uwezekano wa kuanza kuwakopesha vijana walio katika sekta ya kutumia chombo cha pikipiki ya miguu miwili na mitatu," alisema.

Shango alisema kabla ya kuzindua huduma hiyo kwa mkoa wa Mtwara, benki hiyo ilianza kwa kutoa mafunzo kwa viongozi wa madereva wa vyombo vya 'bodaboda na Bajaji' wilaya na mkoa wakiwamo baadhi ya wafanyakazi wa benki hiyo namna ya kusimamia mikopo hiyo ambayo inaenda kutolewa.

Alisema lengo la kutoa elimu ni kuwezesha walengwa kujua ni nini wanatakiwa kufanya ili watakapochukua mkopo huo wa bodaboda au bajaji waweze kupata mafanikio ambayo yamekusudiwa.

Katibu Tawala wa Mkoa Abdallah Malela, alisema huduma ya NMB master loan itasaidia serikali katika kufanya sekta ya usafirishaji kutumia chombo cha bodaboda na bajaji inakuwa rasmi na kufanya vijana ambao walioko kwenye sekta hiyo kutambulika na kuendelea kupata huduma mbalimbali zikiwemo huduma za kifedha.

Malela aliwataka walengwa watakaopata mikopo hiyo kuhakikisha wanatimiza masharti yote ambayo wanatakiwa kufuata na kuwa waaminifu katika kuchukua hiyo mikopo huku akitaka waitumie kuwekeza ili wajiletee maendeleo yaliyokusudiwa.

Ofisa Mkuu Kitengo cha Mikopo NMB, Lola Lema, alisema mkopo wa master boda una riba nafuu na kwamba hauna dhamana na kinachotakiwa ni mlengwa kuonyesha umuhimu wa mkopo huo.

Benki hiyo ya NMB imetenga zaidi ya shilingi bilioni tano kwa ajili ya vijana kwenye sekta ya uendeshaji wa bodaboda na bajaji kwa mwaka wa kwanza na kwamba zaidi ya vijana elfu sabini na tano nchi nzima.

## Wateule tuzo EJAT kutajwa wakati wowote

**Na Elizabeth Zaya**

WATEULE wa umahiri wa uandishi wa habari Tanzania (EJAT) mwaka 2020 wanatarajiwa kujulikana wakati wowote baada ya majaji waliokuwa wamejifungia kwa siku nane kwa ajili ya kupitia kazi zilizowasilishwa na waandishi wa habari kumaliza kazi yao.

Kwa mujibu wa Baraza la Habari Tanzania (MCT), majaji hao walimaliza kazi yao Agosti 19, wilayani Bagamoyo mkoani Pwani.

"Majaji walimaliza kazi hiyo Agosti 19 mjini Bagamoyo walikojichimbia kupitia kazi 395 zilizowasilishwa na wanahabari 147 kuwania tuzo hizo zinazotolewa kuwatambua kwa kazi nzuri kwa mwaka husika," ilieleza taarifa ya MCT.

"Majaji hao wakiwa chini ya Mwenyekiti wao Dk. Joyce Bazira, walifanya kazi hiyo kuanzia Agosti 12 baada ya kuapishwa rasmi na Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili ya MCT, Jaji mstaafu wa Mahakama Kuu, Robert Makaramba Agosti 11, mwaka huu."

Kwa mujibu wa baraza hilo, washindi wa tuzo hizo watatangazwa katika kilele cha mashindano hayo Septemba 10, mwaka huu.

## Ataka vikundi ujasiriamali vitembelewe

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

NAIBU Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Kaspar Mmuya, amewataka viongozi wa kata, wilaya na mkoa kutembelea vikundi vya ujasiriamali vinavyofanya shughuli za uzalishaji wa kujipatia kipato.

Alitoa kauli hiyo jana wakati akikagua miradi ya vikundi vinne vya watu waishio na maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU).

Vikundi hivyo vinasimamiwa na Baraza la Taifa la Watu Waishio na Ugonjwa wa Ukimwi (NACOPHA), vilivyopo katika kata ya Kashai, Buhembe Manispaa ya Bukoba, mkoani Kagera.

Mmuya alisema viongozi hawapaswi kupewa maagizo ya kutembelea vikundi ambavyo vinahitaji uboreshaji wa maisha yao.

Vile vile, Mmuya alisema vikundi vimeonyesha uwezo wa kuanzisha shughuli za ufugaji, kilimo, biashara pamoja na kuchangiana pesa za kusaidia nyakati za shida.

HABARI KIMATAIFA

## Mchakato kuhamisha raia Afghanistan bado mgumu

**Kabul,** AFGHANISTAN

MAREKANI na washirika wake wakati wanaendelea na juhudi za kuwaondoa watu kutoka Afghanistan, mchakato umezidi kuwa mgumu huku tahadhari zikiendelea kutolewa.

Umoja wa Ulaya (EU), umeelezea kwamba huenda itakuwa vigumu kuwasafirisha watu wote kwa wakati uliokusudiwa.

Marekani inalenga Agosti 31, mwaka huu, kuwa siku ya mwisho ya kuwahamisha watu kutoka Afghanistan ingawa mkuu wa sera za nje wa EU Josep Borell alisema, mipango ya kuwahamisha watu 60,000 katika kipindi hicho kifupi haiwezekani.

Siku sita tangu kundi la wanamgambo wa Taliban lilipochukua udhibiti wa Afghanistan, maelfu ya watu wanajaribu kuondoka kutoka katika operesheni ngumu ya kuwahamisha watu katika historia ya miaka ya karibuni.

Picha na mikanda ya video zaonyesha misongamano ya watu kwenye viunga vya uwanja wa ndege mjini Kabul, kitovu cha operesheni hiyo ya kuwaondoa watu inayoendeshwa kwa sehemu kubwa chini ya usimamizi wa Marekani.

Kutokana na hali hiyo ya misongamano mikubwa Marekani na Ujerumani, zimewataka raia wake kuepuka eneo hilo la uwanja wa ndege kwa hofu kwamba hali ya usalama inaweza kuwa hatarishi.

Wakati huo huo, lawama zinatolewa kutoka pande mbalimbali kuhusiana na hali ya Afghanistan.

Rais wa Marekani, Joe Biden, anakabiliwa na ukosoaji unaoongezeka kutokana na video zinazoonyesha vurugu za mara kwa mara, nje ya uwanja wa ndege wa Kabul na pia Waafghanistan, waliojawa na hofu ya kushambuliwa na Taliban wakiomba wasiachwe nyuma. **DW**

# Washindwa kubaini sababu mtoto kuzaliwa na sehemu tatu za uume

**Duhok,** IRAQ

WANASAYANSI wamezidi kushangazwa na kilichosababisha mtoto wa kiume, aliyezaliwa na sehemu tatu za uume, Iraq, miezi kadhaa baada ya kumfanyia operesheni ya kuondoa sehemu mbili.

Tukio hilo wataalamu wanasema ndilo lilikuwa la kwanza kwa binadamu kuzaliwa na sehemu tatu za siri, kitaalamu likiitwa triphallia.

Mtoto huyo alizaliwa akiwa na sehemu tatu za uume katika eneo la Duhok na mara ya kwanza madaktari walimwona akiwa na miezi mitatu.

Tangu kipindi hicho, wanasayansi wamekuwa wakiendelea na utafiti wa kung'amua kwanini alizaliwa na sehemu hizo tatu, ingawa hadi sasa hawajapata majibu.

**Uume wa ziada, au usio wa kawaida ni hali nadra ya kuzaliwa, inayotokea mara moja tu katika kila watoto milioni tano hadi milioni sita.**

Alifanyiwa upasuaji kuondoa sehemu mbili kati ya hizo tatu, ambazo zilikuwa zimeanza kujitokeza katika shina la eneo la korodani.

Sehemu ya tatu ilikuwa katika eneo la kawaida, uume wa mwanamme unapotakiwa kuwapo.

Uchunguzi wa kisa hicho uliochapishwa katika Jarida la Kimataifa la Upasuaji la Novemba mwaka jana, kijana huyo alikuwa akiendelea vizuri katika ziara ya ufuatiliaji mwaka mmoja, baada ya upasuaji.

Uume wa ziada, au usio wa kawaida ni hali nadra ya kuzaliwa, inayotokea mara moja tu katika kila watoto milioni tano hadi milioni sita, wanaozaliwa kulingana na watafiti.

Kiwango cha ukuaji wa sehemu hizo, hutofautiana kutoka mtu mmoja hadi mwingine.

Katika tukio la mtoto huyo wa Iraq, sehemu hizo mbili za ziada zilikuwa na tishu za 'erectile', ziitwayo 'corpus cavernosum' ambazo hujaa damu wakati wa kuamka, na vile vile tishu inayoitwa 'corpus spongiosum' ambayo inasaidia mrija unaotumiwa kupitisha mkojo.

Sehemu hizo za uume wa ziada hazikuwa na mirija ya kupitisha mkojo yaani urethra na ilifanya kuondolewa kwa upasuaji.

"Haijulikani sana juu ya kwanini uume wa ziada huibuka," alisema John Martin, profesa wa anatomia katika Shule ya Tiba ya Chuo Kikuu cha St. Louis. **BBC**




Msururu wa magari ulishuhudiwa katika vituo vya mafuta katika mji wa Beirut, nchini Lebanon, juzi, baada ya nchi hiyo kukumbwa na uhaba wa nishati hiyo kutokana na kuporomoka kwa uchumi. **PICHA: XINHUA**

# UN: Kuna ongezeko la chuki, kutovumiliana

**New York,** MAREKANI

UMOJA wa Mataifa (UN), umesema kuna ongezeko la kauli za chuki, kutovumiliana na hata mashambulio ya mwili kwa watu na vikundi, duniani.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), António Guterres, ameyasema hayo jana katika taarifa ya maadhimisho siku ya kimataifa ya kuwakumbuka waathirika wa vitendo vya vurugu zilizotokana na dini au imani duniani.

Alisema vitendo vya vurugu mara nyingi huambatana na uvunjifu wa haki za kimsingi, ikiwamo haki ya uhuru wa mawazo au dhamira fulani, vinapaswa kubadilika na kuheshimiana.

"Uhuru wa dini au imani ni haki ya binadamu, iliyowekwa katika Hati ya Umoja wa Mataifa na katika Azimio la Ulimwengu la Haki za Binadamu. "Leo, haki hii inajaribiwa. Kwa pamoja tujitolee kuweka ahadi ya kubadili tabia hii na kujenga jamii zinazojumuisha zaidi na zenye amani, ambapo pamoja na utofauti wetu lakini tunatakiwa kusherehekea utajiri ambao unatuimarisha sisi sote."

Guterres alisema janga la Covid-19, limeongeza ubaguzi, kuwatenga na kuwanyima taarifa na mara nyingi walengwa wamekuwa ni vikundi vidogo vya jamii ndogo zenye imani tofauti na inaongeza zaidi muunganiko wa hatari.

"Licha ya hatari, waathirika wanaendelea kupaza sauti zao kwa ujasiri mkubwa kutetea haki zao. Nasimama nao na kuwa na mshikamano nao kamili na kwa juhudi zinazofanywa na asasi za kiraia, jamii na viongozi wa dini katika kuhamasisha kupinga aina yeyote ya kitendo cha vurugu au ubaguzi," alisema Guterres

Akitaja juhudi alizofanya Guterres alisema "Nimefanya jambo hili kuwa moja ya vipaumbele vyangu kwa kufanya mambo kadhaa ikiwamo kupitia mipango mbalimbali kama wito wa kutenda haki za binadamu, mkakati wa Umoja wa Mataifa wa mpango wa utekelezaji juu ya kauli za chuki na Mpango wa Umoja wa Mataifa wa Kulinda Maeneo ya dini."

"Nchi zinajukumu la msingi kwa kuzuia ubaguzi na vurugu na kulinda haki za binadamu na haki ya kuabudu ya jamii ndogo na kuhakikisha wanaotenda vitendo viovu vya uhalifu wanafikishwa katika vyombo vya sheria na kuchukuliwa hatua stahiki." **UN**

MECHI KALI

HOME

WEST HAM

2.52 | 3.43 | 2.72

LEICESTER

AWAY

1 WEKA PESA.
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4 - WEKA PESA.
vodacom m-pesa airtel money tigo pesa EZYPESA
- FUNGUA MENYU YA HALOPESA
- CHAGUA LIPA/LIPIA BILI
- WEKA NAMBA YA KAMPUNI 150888, KUMBUKUMBU 888.
- KISHA WEKA 500 AU ZAIDI.
halopesa
SEND

2 WEKA BET.
- PIGA *150*87#
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE KASINO

# MARTINEZ HANA MPANGO KUONDOKA INTER MILAN



**MILAN,** Italia

INTER Milan inatarajia Lautaro Martinez, kubaki hapo San Siro baada ya kukataa "ofa nzuri" kutoka kwa klabu wapinzani wao, kwa mujibu wa Ofisa Mtendaji Mkuu, Beppe Marotta.

Nerazzurri hao walianza kutetea taji lao la Ligi Kuu ya Italia, Serie A, kwenye ushindi wa mabao 4-0 Jumamosi dhidi ya Genoa.

Usajili mpya wa Hakan Calhanoglu na Edin Dzeko walikuwa miongoni mwa wafungaji, huku kocha, Simone Inzaghi akifurahia ushindi wake wa kwanza.

Antonio Conte, Romelu Lukaku na Achraf Hakimi wote waliondoka hapo Inter, na Martinez pia alikuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka, huku Tottenham ikihusishwa naye. Hata hivyo, raia huyo wa Argentina hakuwa kwenye mchezo huo dhidi ya Genoa, akitoka kushinda Copa America, anaonekana kuwa atabakia hapo Inter.

Akizungumza baada ya mchezo huo, Marotta alibainisha kuwa Martinez alipata ofa kutoka sehemu nyingine, lakini akaamua kubakia hapo.

"Lautaro ni mchezaji mwenye uelewa ambaye ameamua kubakia Inter licha ya kupata ofa nzuri kutoka klabu nyingine," alisema Marotta akiiambia DAZN.



# Benzema yupo sana Real Madrid

**MADRID,** Hispania

NAHODHA wa klabu ya Real Madrid, Karim Benzema ametia saini kuongeza mkataba wa mwaka mmoja utakaombakiza hapo kwenye dimba la Bernabeu hadi mwaka 2023.

Dili hilo litamfikisha mwaka wa 14 tangu ajiunge na klabu hiyo.

Benzema mwenye umri wa miaka 33, aliwasili Bernabeu mwaka 2009 na amefunga mabao 281 katika kipindi cha miaka 11 yakiwamo zaidi ya 20 katika kila misimu mitatu iliyopita ya Ligi Kuu Hispania, LaLiga.

Hatua hiyo ya Benzema kutia saini mkataba mpya inatokana na golikipa Thibaut Courtois kutia saini mkataba mpya wa miaka mitano Real Madrid mapema wiki hii kubaki Bernabeu hadi Juni 2026.

LIVE IN PLAY

BET MECHI IKIENDELEA USHINDE.

SPORTPESA APP

CHEZA, USHINDE. MALIPO FASTA

PAKUA SASA

# KLOPP NA MATUMAINI MKATABA SALAH LIVER



**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, amethibitisha kuwa klabu hiyo imefungua mazungumzo na Mohamed Salah juu ya mkataba mpya wa muda mrefu.

Mkataba wa sasa wa Salah uliosainiwa mwaka 2018, umebaki chini ya miaka miwili, lakini vyanzo vya Liverpool vina hakika makubaliano yatafikiwa.

Nyota huyo wa Misri mwenye umri wa miaka 29, anatarajia kusaini mkataba mpya, baada ya wachezaji wenzake, Trent Alexander-Arnold, Fabinho, Alisson Becker na Virgil van Dijk kufanya hivyo.

Akizungumza baada ya mchezo wa ushindi dhidi ya Burnley Jumamosi, Klopp alisema: "Ninahusika katika kila kitu kinachotokea kwenye klabu.

"Labda mazungumzo mengine hufanyika bila mimi, hiyo inawezekana lakini sina uhakika. Mbali na hayo najua juu ya vitu vyote. "Ni jinsi ilivyo siku zote, hatuzungumzii juu ya vitu hivi. Najua tulibadilisha hilo kidogo na Hendo (Jordan Henderson), lakini hiyo haimaanishi kwamba kuanzia sasa tutawaambia juu ya kila hatua ndogo na mazungumzo.



# *Mbappe aongoza wanaotakiwa United*

**PARIS,** Ufaransa

NYOTA Kylian Mbappe, Erling Haaland na Harry Kane wako kwenye orodha ya malengo ya miamba Manchester United wakati klabu hiyo inataka kufanya usajili mkubwa msimu ujao wa kiangazi.

Tovuti ya michezo, ESPN imeripoti kwamba, Mbappe anafikiriwa kuwa kipaumbele namba moja kule Real Madrid katika uhamisho unaoweza kukamilishwa kabla ya mwisho wa dirisha la usajili Septemba Mosi, mwaka huu, lakini United inafuatilia kwa karibu hatma ya mchezaji huyo.

United inatambua nia ya muda mrefu ya Madrid kwa Mbappe huku maofisa wanasemekana kuwa tayari kutimiza matarajio ya Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 22 ya mshahara mkubwa atakaposajiliwa bila ada ya uhamisho mwaka 2022.

Naye Erling Haaland anaonekana kubaki Borussia Dortmund msimu huu licha ya wakala wake Mino Raiola kufanya mazungumzo na Real Madrid na Barcelona nchini Hispania Aprili mwaka huu.

United pia inatupia jicho uwezekano wa uhamisho wa Harry Kane wa Tottenham Hotspur ambaye hatima yake haijulikani baada ya kuomba kuhamia Manchester City.

MECHI ZA USHINDI


"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 23 - AGOSTI 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 1459 | Bucheon vs Anyang | 3.54 | 3.34 | 1.95 |
| 13:30 | 5916 | Busan I Park vs Sangju Sangmu | 3.43 | 3.19 | 2.04 |
| 16:00 | 2588 | Alashkert Martuni vs Junior Sevan | 2.90 | 2.85 | 2.51 |
| 16:30 | 2940 | Miercurea Ciuc vs Concordia Chiajna | 2.81 | 3.00 | 2.47 |
| 17:00 | 1655 | Rosenborg BK 2 vs Kjelsaas | 5.81 | 4.36 | 1.44 |
| 18:00 | 2057 | Bkma Yerevan vs Urartu | 14.60 | 6.42 | 1.15 |
| 18:30 | 1456 | Montana vs Hebar Pazardzhik | 2.10 | 3.49 | 3.00 |
| 18:30 | 1529 | Radnicki Nis vs Proleter | 1.49 | 3.98 | 5.83 |
| 18:30 | 3447 | Hobro vs Nykobing FC | 2.67 | 3.25 | 2.42 |
| 18:30 | 5345 | CS Mioveni vs U Craiova SA | 3.13 | 2.94 | 2.38 |
| 18:30 | 5471 | Lahti vs HJK Helsinki | 4.46 | 3.44 | 1.72 |
| 19:00 | 1194 | Fredrikstad vs Stjordals-Blink | 1.43 | 4.63 | 5.60 |
| 19:00 | 1476 | OKS Odra Opole vs Chrobry Glogow | 2.24 | 3.23 | 2.95 |
| 19:00 | 2323 | Strommen vs Aalesunds | 4.56 | 3.88 | 1.62 |
| 19:15 | 2257 | Trabzonspor vs Sivasspor | 1.79 | 3.59 | 4.22 |
| 19:30 | 1938 | FK CSKA 1948 II vs Maritsa Plovdiv | 5.20 | 4.14 | 1.51 |
| 19:30 | 3600 | Fortuna Hjorring W vs Aalborg BK | 1.11 | 7.33 | 17.37 |
| 19:30 | 4162 | FK Lviv vs FC Ingulets | 2.24 | 3.18 | 2.99 |
| 19:30 | 4625 | Cagliari vs Spezia | 1.94 | 3.63 | 3.78 |
| 19:45 | 1438 | Chateauroux vs Le Mans | 2.43 | 2.88 | 3.07 |
| 20:00 | 1068 | Ismaily SC vs Talaea El Gaish | 2.31 | 2.91 | 3.35 |
| 20:00 | 2826 | Nordsjalland vs Vejle BK | 1.75 | 3.66 | 4.35 |
| 20:00 | 3121 | Vilafranquense vs Covilha | 2.78 | 2.88 | 2.64 |
| 20:00 | 3994 | Ostersunds vs Kalmar | 3.83 | 3.25 | 1.90 |
| 20:00 | 4231 | Helsingborg vs Vasalunds IF | 1.53 | 4.40 | 5.60 |
| 20:00 | 4431 | Norrby IF vs Akropolis IF | 1.67 | 3.86 | 4.91 |
| 20:00 | 4471 | Djurgardens IF vs Mjallby | 1.37 | 4.55 | 6.77 |
| 20:00 | 5282 | Pfk Botev Plovdiv II vs Yantra Gabrovo | 1.87 | 3.73 | 3.44 |
| 20:00 | 5575 | IFK Goteborg vs Varbergs Bois | 1.80 | 3.34 | 4.16 |
| 21:00 | 1108 | Leiknir vs HK Kopavogs | 2.62 | 3.39 | 2.39 |
| 21:00 | 1917 | Jong AZ Alkmaar vs FC Oss | 2.44 | 3.22 | 2.74 |
| 21:00 | 2106 | UMF Selfoss W vs IBV Vestmannaeyjar W | 1.62 | 4.06 | 4.35 |
| 21:00 | 2702 | Ranheim vs Ham-Kam | 1.99 | 3.87 | 3.00 |
| 21:00 | 3091 | Excursionistas vs El Porvenir | 1.85 | 3.19 | 4.16 |
| 21:00 | 3526 | Getafe vs Sevilla FC | 3.46 | 3.06 | 2.28 |
| 21:00 | 4693 | Pacos Ferreira vs GD Estoril | 2.22 | 3.06 | 3.36 |
| 21:00 | 5295 | Mirandes vs Amorebieta | 2.15 | 2.96 | 3.66 |
| 21:00 | 5465 | CS Petange vs FC Rodange 91 | 1.85 | 3.58 | 3.63 |
| 21:00 | 5614 | Jong PSV vs FC Eindhoven | 2.45 | 3.34 | 2.65 |
| 21:30 | 1027 | Podbeskidzie Bie vs Skra Czestochowa | 1.41 | 4.45 | 6.19 |
| 21:45 | 1018 | Sampdoria vs AC Milan | 3.81 | 3.61 | 1.94 |
| 21:45 | 2592 | Galatasaray vs Hatayspor | 1.47 | 4.44 | 5.92 |
| 21:45 | 2598 | AJ Auxerre vs Guingamp | 2.03 | 3.16 | 3.75 |
| 22:00 | 1086 | West Ham vs Leicester | 2.52 | 3.43 | 2.72 |
| 22:00 | 3814 | Al Masry Club vs Enppi Club | 2.11 | 2.97 | 3.81 |
| 22:15 | 2565 | Njarovik vs Haukar | 1.76 | 4.16 | 3.48 |
| 23:00 | 3287 | Leganes vs Burgos | 1.69 | 3.40 | 5.32 |
| 23:00 | 4671 | Osasuna vs Celta Vigo | 2.70 | 3.10 | 2.75 |
| 23:15 | 1809 | Boavista vs Santa Clara | 2.22 | 3.06 | 3.36 |
| 23:30 | 3686 | Alianza Lima vs Sport Huancayo | 1.81 | 3.05 | 4.65 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ULAYA




# GUARDIOLA AKUNWA NA KIWANGO CHA JESUS CITY

Anafuraha kucheza kushoto, kulia au katikati, hana tabia ya kulalamika, akicheza dakika...

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amesifia kiwango cha Gabriel Jesus wakati Manchester City ikiibuka na ushindi wa mabao 5-0 dhidi ya Norwich City na amesema anajisikia mtu mwenye bahati kufanya kazi na mchezaji huyo wa Brazil.

**Jesus alianza kwa City katika mchezo huo wakati kulikuwa na mabadiliko matatu kutoka kwenye mchezo uliopita walipoteza dhidi ya Tottenham.**

Jesus alianza pamoja na Ferran Torres na Jack Grealish kwenye mchezo huo wa Jumamosi pale katika dimba la Etihad.

Licha ya Jesus kutofunga kwenye mchezo huo, lakini alitoa mchango mkubwa kwenye mabao matatu, ikiwamo pasi za mwisho kwa Jack Grealish na Raheem Sterling. Na Guardiola baada ya mchezo huo, alimsifia Jesus na kusema kwamba ameonyesha kiwango cha juu zaidi.

"Kama mtu anastahili heshima na kuwa nyota wa mchezo, yeye ndio anafaa kwa zawadi hiyo. Mama na baba yake wanatakiwa kujisikia fahari kuwa na mtoto kama yeye," alisema Guardiola akiiambia BBC Sport.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya mchezo huo, kocha huyo kutoka Catalunya, alisema: "Yeye ni mchezaji ambaye anapenda kujitafutia nafasi nzuri.

"Moja ya sababu ya mimi kuwa kocha ni kufanya kazi na watu wazuri kama Gabriel. Kamwe hajawahi kulalamika, akicheza dakika tano zinakuwa bora zaidi.

"Anafuraha kucheza kushoto, kulia au katikati na leo (juzi) alikuwa na wakati mzuri zaidi kwa ushirikiano na Kyle (Walker).

"Nimefurahishwa na kiwango chake alihusika katika mabao yetu matatu ni mchezaji muhimu sana kwetu."

## ZISIKUPITE

### BECKHAM NA MESSI MIAMI

DAVID Beckham amefanya mazungumzo na Lionel Messi juu ya kujiunga na Inter Miami wakati mkataba wa mshambuliaji huyo wa Argentina na PSG utakapomalizika mwaka 2023. ***(Mirror)***

### RICE HANA FURAHA WEST HAM

KIUNGO wa kati wa West Ham na England, Declan Rice, 22, hafurahia gharama ya pauni milioni 100 ambayo klabu imemuwekea, ikimfanya asiweze kuondoka katika msimu huu wa majira ya joto. ***(Sunday Telegraph)***

### SILVA ATAKIWA AC MILAN

KLABU ya AC Milan inataka kumsajili kiungo wa Manchester City na Ureno, Bernardo Silva, 27, kwa dau la pauni milioni 45. ***(Star on Sunday)***

### VLAHOVIC ATEGWA SPURS

MSHAMBULIAJI wa Fiorentina na Serbia, Dusan Vlahovic analengwa sana na Tottenham ikiwa Harry Kane ataondoka msimu huu wa majira ya joto. ***(La Repubblica)***

### BAKAYOKO AKARIBIA MILAN

AC Milan wanakaribia kukamilisha mpango wa kumnunua kiungo wa kati wa Chelsea Mfaransa Tiemoue Bakayoko, 27. ***(Calciomercato)***

### AZIITA MADRID, BARCA

TANGUY Ndombele anataka kuhamia Real Madrid, Barcelona au Bayern Munich kama akiondoka Tottenham. ***(AS)***

### JUVENTUS, SPURS WATETA

MKURUGENZI wa Soka wa Tottenham, Fabio Paratici amefungua mazungumzo na Juventus juu ya uhamisho wa Tanguy Ndombele, katika makubaliano ya kubadilishana ambayo yatafanya kiungo wa Marekani, Weston McKennie mwenye umri wa miaka 22, ajiunge na klabu hiyo ya London kaskazini. ***(Tuttosport)***

### SARR KUNG'OLEWA CHELSEA

KLABU ya Everton imejiunga na Bologna na Eintracht Frankfurt katika harakati za kuwania saini ya mlinzi wa Ufaransa, Malang Sarr mwenye umri wa miaka 22, kutoka Chelsea. ***(Gianluca Di Marzo)***

### NEVES BADO LULU UNITED

KLABU ya Manchester United bado inavutiwa na mchezaji wa Wolves na kiungo wa kati wa Ureno, Ruben Neves. ***(Sunday Express)***

### ANUKIA NEWCASTLE

NEWCASTLE itafanya mazungumzo na Everton juu ya uhamisho wa kiungo wa Colombia, James Rodriguez mwenye umri wa miaka 30, kwa ombi la kocha, Steve Bruce. ***(Calcio In Pillole, via Star)***

## Azam yafuata nne za kirafiki Zambia

**Na Saada Akida**

KIKOSI Cha Azam FC kinaondoka leo kuelekea Ndola nchini Zambia kwa ajili ya kambi ya wiki moja na nusu na kucheza mechi nne za kirafiki kujiandaa na mchezo wao wa Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Horseed SC.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Ofisa Habari wa timu hiyo, Zakaria Thabiti 'Zaka za Kazi', alisema lengo la kuhamishia kambia hiyo Zambia ni ili kucheza mechi hizo nne za kirafiki kwa ajili ya kujiandaa na michuano hiyo inayotarajiwa kuanza Septemba 10, mwaka huu.

Alisema maandalizi ya safari hiyo yamekamilika na leo wanatarajia kuondoka na wachezaji wote walioingia kambini, isipokuwa Prince Dube ambaye alikuwa katika matibabu na anatarajia kuungana na wenzake nchini Zambia Jumatano wiki hii.

"Dube alikuwa majeruhi na alipewa mapumziko ya wiki nne, tunatarajia kuwa naye Zambia katika maandalizi yetu ya michuano hiyo ya kimataifa pamoja na Ligi Kuu Tanzania Bara," alisema.

## Stars kambini kesho kuiwinda DR Congo

**Na Saada Akida**

TIMU ya Taifa ya Tanzania 'Taifa Stars' inatarajia kuingia kambini kesho na Jumatano kuanza mazoezi rasmi kujiandaa na michezo miwili ya kuwania kufuzu Kombe la Dunia dhidi ya DR Congo na Madagascar.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Kim Poulsen, wakati wakiendelea na mazoezi, Shirikisho la Soka nchini (TFF), litakuwa likipambana kutafuta timu ya kucheza nayo mechi ya kirafiki kabla ya kwenda DR Congo.

Alisema wana muda mfupi wa maandalizi, lakini kulingana na kikosi cha wachezaji aliowaita, ana matarajio makubwa ya kufanya vizuri katika michezo hiyo miwili dhidi ya DR Congo watakaocheza ugenini na Madagascar ambao utapigwa kwenye dimba la Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

"Muda ni mfupi tunalazimika kujiandaa vizuri, TFF wanapambana kutafuta, nchi za jirani kuweza kupata 'match fitness' kabla ya kwenda DR Congo, ninamatarajio makubwa ya kufanya vizuri katika mchezo huo na hata wa hapa nyumbani," alisema Poulsen.

# WATATU TU KUTUWAKILISHA OLIMPIKI NI AIBU - SAMIA

**Na Adam Fungamwango**

RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suhulu Hassan, ameonyesha kusikitishwa na nchi kuwakilishwa na wachezaji watatu pekee kwenye michuano ya Olimpiki iliyomalizika hivi karibuni, Tokyo nchini Japan.

**Kwenye halfa iliyofanyika jana Ikulu, Dar es Salaam ya kuwapongeza wanariadha hao watatu walioiwakilisha nchi kwenye michuano hiyo, pamoja na timu ya Taifa ya Vijana chini ya miaka 23, iliyotwaa Kombe la CECAFA nchini Ethiopia mwishoni mwa mwezi uliopita.**

Rais pia alishangaa idadi ya viongozi kuwa kubwa zaidi kuliko wachezaji.

"Tunaenda na wachezaji watatu na viongozi 11. Tutaenda kushiriki au tunaenda kutembea? Angalau basi viongozi 11, wachezaji sita. Naomba turekebishe. Siwalaumu, lakini naomba tujirekebishe."

Rais Samia, alianza kuwapongeza wanamichezo wote kwa hatua waliofikia na kuitangaza nchi kimataifa.

"Lakini pamoja na pongezi hizo, ukweli ni kwamba kwa taifa kubwa kama letu, kuwakilishwa na wachezaji watatu au wachache kwenye michezo mbalimbali duniani ni aibu kubwa. Tanzania tunaweza kuzalisha wachezaji wengi.

Kwa mfano kwenye Olimpiki waliotuwakilisha ni majeshi. Kuna na wengine, twendeni tufanye kazi na maeneo ya sekta ambazo tunahisi huko tutatoa wanamichezo wengi wazuri watakaotuwakilisha," alisema Rais akitoa mfano majeshini mbali na Simbu, lakini wanaweza kuibuliwa wanamichezo wengine wakaiwakilisha nchi hapo baadaye ili kuepukana na kupeleka wachezaji wachache.

" Tufanye kazi na jeshi letu kwenye sekta ya michezo, tuwaibue wanamichezo walioko kule, tuwawatengeneze waende wakatuwakilishe.

"Lakini kuna mikoa ambayo tunaijua tunaweza kutoa wenye mbio nyingi, Manyara na Arusha. Kina Simbu wangekuwa wanne, mmoja angechukua ya tatu, mwingine ya pili na mwingine. Tuwaangalie wenzetu Ethiopia na Kenya, mchezo mmoja wanashindana wanne, wanasaidiana," alisema Rais.

Aliongeza kuwa wanapokuwa wachezaji wengi kwenye mchezo mmoja husaidiana kwa namna moja ama nyingine, angalau mmoja awe wa kwanza, lakini anapokuwa mmoja kunakuwa hakuna wa kumsaidia wala kumpa moyo mwenzake.

Mbali na Simbu, Tanzania iliwakilishwa na Gabriel Geah na Failuna Abdi.

# Tamasha la Zuchu lapagawisha Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MCHEZA kwao hutuzwa! Hivyo ndivyo unavyoweza kueleza jinsi tamasha la Zuchu Home Coming na Zantel, lilivyokonga nyoyo za watu wengi katika Uwanja wa Amaan mjini Zanzibar juzi usiku.

Tamasha hilo lililofanyika jana lilipambwa na wasanii wa muziki kutoka Zanzibar 'Zenjifleva' akiwamo Sultan King, Berry black, Cholo na Malkia wa Mipasho, Khadija Kopa, pia lilishuhudiwa na wasanii wa Bongo Fleva akiwamo Mr. Blue, Lavalava, Mbosso, Chege, Jux, Luludiva na Queen Darleen wakitoa burudani.

Moja ya wasanii walioonekana kukonga nyoyo za wengi ni pamoja na mama mzazi wa Zuchu, Khadija Kopa ambaye alitumbuiza kwa miondoko ya Taarabu na kupata shangwe kubwa kutoka kwa watu waliokuwapo uwanjani hapo.

Zuchu alianza kwa kutumbuiza nyimbo zake maarufu ikiwamo wimbo wa Itawachoma, Nisamehe na baadaye kuhitimisha kwa shangwe kubwa alipoimba wimbo wake wa Sukari.

Awali, Mkuu wa Kitengo cha Biashara na Masoko wa Zantel, Aneth Muga, alisema tamasha hilo pamoja na mambo mengine lililenga kutambua vipaji mbalimbali vya muziki kwa kuwapa wasanii hasa wachanga nafasi ya kuonyesha vipaji vyao.

Huu ni mwendelezo wa Kampeni yetu ya Pasua Anga Ki-Zantel 4G, ambayo inalenga kutoa elimu juu ya umuhimu wa mtandao wa 4G katika kuleta manufaa ya kijamii na kiuchumi.

"Sote tunafahamu kwamba Zuchu ni mtoto na kipaji wa nyumbani kwetu Zanzibar, na kupitia tamasha hili Zuchu anarudi nyumbani kwa kutoa burudani ya aina yake hapa Uwanja wa Amani. Pia, kupitia tamasha hili, wanamuziki wa Zenjifleva watapata nafasi ya kuonyesha vipaji vyao ili na wao waweze Kupasua Anga kama ambavyo Zuchu amefanya," alisema.



Mkuu wa Kitengo cha Biashara na Masoko wa Zantel, Aneth Muga, akizungumza na waandishi wa habari wakati wa ufunguzi wa tamasha la Zuchu Home Coming na Zantel juzi katika Uwanja wa Amaan Zanzibar. Tamasha hilo lilihusisha wasanii mbalimbali wakiwamo wa Zenjifleva na Bongo Fleva. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Michezo

Jumatatu Agosti 23, 2021
Nipashe



Guardiola akunwa na Jesus City UKURASA 22

# Sven amtaja Sakho, ubora kikosi Simba

## ●●● Akunwa pia na nyota wapya vijana, Gomes naye...

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya kumshuhudia kiungo mpya wa Simba, Msenegal Pape Ousmane Sakho, akiichezea timu yake ya Simba kwa mara ya kwanza katika mechi ya kirafiki dhidi ya FAR Rabat juzi, Kocha Mkuu wa miamba hiyo ya Morocco, Sven Vandenbroeck, amesifu ubora wa mchezaji huyo na kumtabiria makubwa ndani ya kikosi hicho.

**FAR Rabat, inayonolewa na kocha huyo wa zamani wa Simba, ilicheza mechi ya kirafiki ya kujiandaa na msimu mpya dhidi ya mabingwa hao wa Ligi Kuu Bara na kulazimishwa sare ya mabao 2-2 juzi nchini Morocco.**

Simba ambayo imeweka kambi nchini humo ikijiandaa na msimu mpya, kwa sasa kikosi chake kimeongeza nyota 10 wapya katika dirisha hili la usajili na wote wapo kambini nchini Morocco wakiendelea kujifua na kikosi hicho kitakachopeperusha bendera ya Tanzania kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Tayari Simba ambayo imewapoteza viungo wake wawili, Luis Miquissone anayetarajiwa kutua Al Ahly ya Misri na Clatous Chama aliyejiunga na RS Berkane ya Morocco, imesajili wachezaji wapya watano wakigeni ambao ni viungo Wamalawi wawili, Peter Banda na Daucan Nyoni, kiungo raia wa Mali, Sadio Kanoute, Sakho na beki Mkongomani Henock Inonga Baka 'Varane'.

Wachezaji wengine wapya waliosajiliwa katika kikosi hicho ni Watanzania; mshambuliaji Yusuph Mhilu, beki wa pembeni Israel Mwenda, kiungo Jimmyson Mwanuke na Abdulsamad Rabiu.

Akizungumzia mchezo huo baada ya mechi hiyo ya kirafiki, Sven ambaye ni raia wa Ubelgiji, alisifu ubora wa wachezaji wapya waliosajiliwa na timu hiyo kwamba ni wenye morali ya kupambana uwanjani.

"Nimeiona Simba yenye mabadiliko kwenye kikosi, wachezaji wenye umri mdogo na wenye morali ya kupambania timu, kuna mfungaji wa bao la pili (Papa Ousmane Sakho) ni mchezaji bora sana, nadhani atakuwa na mchango mkubwa kwenye timu," alisema Sven.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Simba, Mfaransa Didier Gomes, aliwataka mashabiki wa klabu hiyo kuwa wavumilivu kwa kuwa bado kikosi chake kinahitaji kuendelea kuimarika na anaamini kinaweza kufanya vizuri zaidi kadri anavyokiandaa.

"Tunahitaji kuendelea kuimarika na naamini kikosi hiki kinaweza kufanya vizuri zaidi. Tunapaswa kuwa wavumilivu, bado tuna mwezi mmoja wa kujiandaa na nina uhakika timu itakuwa tofauti kabisa baada ya wiki mbili, naiamini timu yangu," alisema.

Kwa upande wa Meneja wa timu hiyo, Patrick Rweyemamu, alisema wanafanya mazoezi mara mbili kwa siku na katika mchezo wao wa kirafiki wa juzi ulikuwa ni kama mechi ya kujifua kwa sababu haukuhusisha sana mashabiki.

Alisema walichotaka kukiona katika mchezo huo ni kutazama zaidi kile wachowafundisha wachezaji mazoezini kama wanaweza kukifanyia kazi uwanjani.

Aidha, Rweyemamu alisema mazoezi yanaendelea vizuri na kumeanza kuwa na mabadiliko makubwa kikosini ingawa sasa kumeanza kujitokeza changamoto ya kuwakosa baadhi ya wachezaji wao walioitwa timu zao za taifa.

"Kwa sasa changamoto kubwa tunayoendelea nayo ni kikosi kupungua, timu yetu ina wachezaji wengi wa timu ya taifa, tayari wameanza kupungua kurudi timu zao za taifa, lakini tunaendelea kujipanga kuona tunaweza vipi kulihimili hilo ili tuweze kuendelea na mazoezi na kila kitu kiende vizuri," alisema Rweyemamu ambaye kitaaluma ni kocha.



Kiungo mpya wa Simba, Sadio Kanoute, akiwa mazoezini na timu hiyo nchini Morocco. **PICHA: SIMBA**

# Rais Samia kudhamini CECAFA Wanawake

**Na Adam Fungamwango**

RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, amekubali kuwa mdhamini wa michuano ya Kombe la CECAFA Wanawake, linalozishirikisha timu za nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, zilizo chini ya Baraza la Vyama vya Soka vya ukanda huu.

Akizungumza jana Ikulu, Dar es Salaam kwenye halfa ya kuipongeza timu ya Taifa ya Vijana chini ya miaka 23 iliyotwaa Kombe la CECACA kwa umri huo Julai 30, mwaka huu nchini Ethiopia, pamoja na wanariadha walioiwakilisha Tanzania kwenye michuano ya Olimpiki hivi karibuni, Tokyo nchini Japan, Rais Samia alisema amekubali kuwa mdhamini baada ya ombi la Rais wa Shirikishisho la Soka nchini ambaye ni Rais wa sasa wa CECAFA, Wallace Karia kutaka kufanya hivyo, kama ambayo Rais Paul Kagame amekuwa akidhamini michuano ya Kombe la CECAFA kwa Klabu Bingwa za Ukanda huu, na kupachikwa jina la Kombe la Kagame.

"Kuna ombi tulinong'ona na Mheshimiwa Rais wa TFF, wanataka kuanzisha CECAFA ya Wanawake, lakini mashindano haya wanataka udhamini, akanitolea mfano mwenzako Kagame anadhamini michuano fulani huko, sasa itakuwa vema na wewe ukadhamini haya," alisema Samia na kuongeza.

"Nikamuuliza hebu niambie kiasi gani niangalie misuli yangu, akanitajia hicho kiasi ambacho sitaki kukisema hapa, lakini nimepima misuli yangu, nikaona mwenyewe sitaweza, lakini nitajua nitakapozipata.

Kwa hiyo niwatangazie kuwa nitadhamini haya mashindano," alisema na kusababisha waliohudhuria hafla hiyo kupiga makofi kuonyesha kufurahi kwa kukubali ombi hilo.

Mbali na hilo, Rais aliipongeza timu ya Taifa ya Vijana U-23 kwa kuchukua Kombe la CECAFA, pamoja na wanariadha wa Tanzania walioiwakilisha nchini kwenye michuano ya Olimpiki mwaka huu huko Tokyo nchini Japan.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >